

Mhh! Gigy Money sijui atakuelewa mchungaji

UKURASA 20




Solskjaer: Najua Pogba hana furaha

UKURASA 21

MAISHA
Nipashe Jumapili
Baba, Mama na Mwana



HARUSI



MAISHA NI NYUMBA
Jinsi ya kusafisha choo na bafu katika nyumba



Namna ya kuandaa saladi ya Sausage



Papai linatosha kukamilisha ndoto zako


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Novemba 22, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580407

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## MATOKEO DARASA LA 7

# NI MADUDU YA KUTISHA



• **Mwalimu** wa taaluma abambwa chooni akigawa majibu, walimu wakuu 38 matatani udanganyifu wa mitihani... *Endelea uk. 2 & 3*

## YALIYOMO


UKURASA WA 2
AJALI SCANIA, SEMI TRELA YAUA WATU WATANO

UKURASA WA 3
WAFUNGWA WALIOMPORA SILAHA ASKARI, KUMJERUHI WAKAMATWA


## Dk. Mwinyi awatwisha zigo zito mawaziri

UKURASA 4



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Tabia Mwita Maulid, kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, wakati wa hafla ya kuapisha Baraza jipya la Mawaziri, katika viwanja vya Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


## Vigogo 40 matatani kwa ujenzi nyumba ufukweni

UKURASA 2


**MICHEZO** YANGA, NAMUNGO MECHI YA HESABU UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Madudu ya kutisha mtihani darasa la saba

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani Tanzania (NECTA), limetangaza matokeo ya darasa la saba, huku likieleza kuwapo kwa udanganyifu mkubwa, ikiwamo mwalimu wa taaluma akikutwa chooni akigawa majibu kwa wanafunzi.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alisema jana wakati akitangaza matokeo hayo mbele ya waandishi wa habari kuwa udanganyifu huo umefanywa na walimu wakuu wa shule 38, hivyo kusababisha matokeo ya wanafunzi 1,059 kufutwa. Dk. Msonde alisema ufaulu kwa mwaka huu umeongezeka na kufikia asilimia 82.68, ikilinganishwa na mwaka jana uliokuwa asilimia asilimia 81.50.

Alisema watahiniwa 833,672 kati ya 1,008,307 wamefaulu kwa kupata asilimia 100 au zaidi ya alama 250 sawa na asilimia 82.68, kwamba wasichana ni 523,760 na wavulana ni 484,547.

"Kati yao waliofaulu kwa asilimia hizo wasichana ni 430,755 sawa na asilimia 82.24 na wavulana ni 402,917 sawa na asilimia 83.15. Mwaka 2019, waliofaulu walikuwa asilimia 81.50, hivyo kuna ongezeko la ufaulu kwa asimilia 1.18," alisema Dk. Msonde.

**UDANGANYIFU**

Aidha, Dk. Msonde alieleza baadhi ya shule zilivyofanya udanganyifu wakati wa kufanyika mtihani, ikiwamo Shule ya Msingi Dominion, iliyoko mkoani Arusha.

Dk. Msonde alisema siku ya kufanyika mtihani, Oktoba 8, mwaka huu, Ofisa wa NECTA alishuhudia wanafunzi wa shule hiyo kwa nyakati tofauti, wakitumia choo kimoja bila kujali jinsia.

"Ofisa wetu alipoingia katika choo hicho alimkuta mwanamume akiwa amevaa mavazi ya upishi akiwa amekaa huku mkononi akiwa na majibu ya mtihani wa maarifa ya jamii, ambayo alikuwa akiwapa wanafunzi waliokuwa wakiingia katika choo hicho, alikuwa mwalimu wa taaluma, Shamsidini Ahmed wa shule hiyo," alisema Dk. Msonde na kuongeza:

"Wakati akikamatwa, alitaka kupoteza ushahidi kwa kutaka kutumbukiza karatasi za majibu chooni lakini hakufanikiwa. Alikamatwa na kufungiwa kwenye ofisi," alisema Dk. Msonde.

Baada ya mtihani kumalizika, alisema walipofungua mlango ili kumkamata hakuwapo, lakini dari na bati katika chumba hicho walikuta vimefumuliwa. Hata hivyo, alisema mwalimu huyo alikamatwa baadaye.

Alisema udanganyifu mwingine ulihusisha wakuu wa shule, askari mgambo na wasimamizi ambao waliandaa vikundi vya watu wakiwamo wahitimu wa sekondari, ambao walikuwa wakiwafanyia mtihani wanafunzi.

Dk. Msonde alitaja shule na idadi ya waliokamatwa kwenye mabado kuwa ni Halmashauri ya Gairo (11), Mvomero (12) mkoani Morogoro, Bariadi mkoani Simiyu, waliokamatwa ni (13) kutoka shule tatu tofauti.

"Halmashauri ya Sikonge mkoani Tabora (11), Halmashauri ya Moshi mkoani Kilimanjaro (5), Jiji la Arusha (5), Halmashauri ya Tandahimba mkoani Mtwara (7), Halmashauri ya Kiteto mkoani Manyara (4), Halmashauri ya Buchosa mkoani Mwanza (3).

Dk. Msonde alisema wakati wa usahihishaji walizibaini shule 19 zilizopo mikoa ya Simiyu, Geita, Morogoro, Arusha na Tabora zilikuwa na mfanano wa majibu, kwa kuwezeshwa na walimu wakuu na wasimamizi wa mitihani wa shule zao.

Alisema matokeo yenye udanganyifu yamefutwa na wanafunzi hao hawatafanya mtihani tena.

Katika mtihani wa kidato cha nne unaotarajia kufanyika kuanzia kesho, wamebaini kuwa mpaka sasa kuna shule 71 ambazo ziko katika mchakato wa kufanya udanganyifu na wamezipa onyo.

Aidha, alieleza kuwa NECTA imezuia matokeo ya watahiniwa 110 kutokana na matatizo mbalimbali yaliyowakuta, kupewa nafasi ya kuufanya tena mwakani.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akikagua eneo utakapojengwa mradi wa Bwawa la Maji Farkwa, wilayani Chemba, mkoani Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Ajali Scania, semi trela yaua watano

**Na Lulu George,** HANDENI

WATU watano wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa baada ya magari mawili kugongana na kuwaka moto, katika Kata ya Kitumbi wilayani hapa usiku wa kuamkia jana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema ilitokea juzi majira ya saa 5:00 usiku na kuhusisha gari lenye namba za usajili T988 na tela lenye namba T 757 CGC aina ya Scania, lililokuwa likiendeshwa na Seleman Muya (32), mkazi wa Tanga.

Alisema gari hilo lilikuwa limepakia saruji kutoka Tanga kwenda Dodoma likiwa na abiria wawili ambao ni Bakari Tendwa mkazi wa Tanga na abiria mwingine hajafahamika majina yake.

Alisema gari lenye namba za usajili T 895 DMD aina ya Canter lililokuwa linaendeshwa na dereva aliyefahamika kwa jina moja la Rashid, akitokea Dar es Salaam kwenda Tanga akiwa na utingo wawili ambao wote wamefariki dunia.

Kamanda Chatanda alisema utingo hao waliofahamika kwa jina moja moja la Mujibu (28) na Dominic (20) wote ni wakazi wa Lushoto.

"Baada ya magari kugongana yote mawili yaliwaka na kuteketea kwa moto na kusababisha vifo vya dereva na utingo wote waliokuwa kwenye canter pia kusababisha vifo kwa dereva wa semi na abiria mmoja ambaye hajafahamika. Majeruhi Bakari Tendwa ambaye ameungua moto kidogo maeneo ya kichwani na kuvunjika mguu wa kushoto," alisema.

Kamanda Chatanda alisema majeruhi amelazwa Kituo cha Afya Mkata, huku miili ya marehemu ikiwa imehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti cha kituo hicho kwa ajili ya utambuzi na uchunguzi wa daktari.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa Canter kutaka kulipita gari lingine, wakati eneo hilo halifai kwa kupishana, hivyo kugongana na lori.

# Vigogo 40 matatani kwa kujenga ufukweni

**Na Sanula Athanas,** MWANZA

BAADHI ya matajiri wa Kanda ya Ziwa, wameingia matatani kutokana na kujenga majengo ya kifahari kwenye fukwe za Ziwa Victoria, Nipashe inaripoti kutoka Mwanza.

Katika semina maalum kwa wahariri juu ya Ushiriki wa Vyombo vya Habari Kuhusu Usimamizi wa Rasilimali za Maji katika Bonde la Ziwa Victoria iliyofanyika jijini Mwanza juzi, uongozi wa Bodi ya Maji katika bonde hilo ilifichua kuwapo kwa dosari ya vigogo hao kujenga nyumba za mabilioni ya shilingi kwenye fukwe hizo.

Ogoma Mangasa, Mkuu wa Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini wa bodi hiyo, alisema tayari uongozi wa bodi umeandika barua kwa vigogo hao kuzuia maendeleo ya uwekezaji kwenye eneo hilo ili kulinda usalama ziwa hilo.

"Vigogo zaidi ya 40 hadi sasa tumewaandikia barua kuhusu suala hili. Wako katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Geita," alibainisha Mangasa.

Hata hivyo, kiongozi huyo alianika ugumu unaowakabili katika kutekeleza majukumu yao ikiwamo kuwadhibiti vigogo hao wanaovamia na kuendeleza maeneo ya Ziwa Victoria, akiwataja wanasiasa kuwa sehemu ya mzizi wa matatizo.

Kiongozi huyo pia alisema uvamizi wa maeneo hayo ya ziwa unachochewa na baadhi ya mamlaka za serikali kutoa vibali vya ujenzi kwenye maeneo hayo ambayo kisheria hayaruhusiwi kuendelezwa.

"Baada tu ya kuwa tumeandika hizo barua, kelele nyingi zimepigwa kwa sababu ukigusa tu suala la maji na ulinzi wa vyanzo vyake, tayari unamtekenya kila mtu.

"Lakini wengi wameitikia wito akiwamo Mzee... (alimtaja mmoja wa mabilionea jijini hapa). Ambao hawajaitikia ni wale ambao wana 'legal documents' (nyaraka za kisheria) kutoka mamlaka zingine za serikali.

"Tumefanya kazi kwa karibu na NEMC (Baraza la Taifa la Uhifadhi Mazingira) lakini tumepata shida kidogo na watu wa ardhi kutoka Jiji. Wametoa vibali vya ujenzi kwenye maeneo ambayo kisheria hayaruhusiwi kuendelezwa. Wao wamejali zaidi mapato ya jiji.

"Mpaka sasa, sisi hatujashindwa, tuko katika mazungumzo na hizo mamlaka zingine za serikali. Tukishindwa, tutaliwasilisha suala hili kwa Katibu Mkuu wa wizara ili lishughulikiwe na mamlaka za juu zaidi. Tunatafuta namna bora ili tusiumize upande wowote maana kuna hao waliopewa vibali na mamlaka za serikali, ukikurupuka kutoa uamuzi, unaweza kuitia hasara kubwa serikali," Mangasa alifafanua.

Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009, inapiga marufuku kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji.

Alisema ujenzi huo holela pia umekuwa chanzo cha mafuriko katika Jiji la Mwanza, yakiwamo yaliyotokea mwezi huu jijini.

Katika semina hiyo, Mangasa pia alizungumzia tatizo la uchimbaji holela wa visima vya maji, alibainisha kuwa linasababishwa na kukosekana kwa elimu ya uhifadhi na matumizi ya vyanzo vya maji.

# Ufaulu somo la Kiingereza waporomoka

Na Romana Mallya

WAKATI Herrieth Josephat kutoka Shule ya Msingi Graiyaki ya mkoani Mara akiibuka mwanafunzi bora kitaifa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, ufaulu somo la Kingereza umeshuka kwa asilimia 19.39.

Mwaka jana ufaulu wa somo hilo ulikuwa asilimia 76.63 lakini kwa mwaka huu umefikia asimilia 57.24.

Akitangaza matokeo ya mtihani huo jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Charles Msonde, alisema wakati ufaulu wa somo hilo ukishuka, ufaulu wa Kiswahili umepanda na kufikia asilimia 87.68. Msonde alisema takwimu zinaonyesha ufaulu umepanda kati ya asilimia 0.43 hadi asilimia 5.10 katika masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Maarifa ya Jamii, ikilinganishwa na mwaka jana.

“Somo la Hisabati na Sayansi ufaulu wake umeshuka kidogo kwa asilimia 0.33 na asilimia 0.65 mtawalia ikilinganishwa na mwaka jana,” alisema.

**KUMI BORA KITAIFA**

Dk. Msonde aliwataja na shule zao kwenye mabano kuwa ni Herieth Josephat (Graiyaki, Mara), Huma Masala (Kwema Modern, Shinyanga), Gregory Alphonce (Twibhoki, Mara) na Nyambina Musa (Graiyaki, Mara).

Wengine ni Andrew Mabula (Kwema Modern, Shinyanga), Jonas Ayubu (Little Flower, Mara), Emmanuel Marwa (Kwema Modern, Shinyanga), Prosper Tumbo na Yesaya Bendera nafasi ya kumi wote kutoka shule ya God's Bridge mkoani Mbeya.

**WASICHANA 10 BORA KITAIFA**

Aliwataja na shule zao kwenye mabano kuwa ni Harieth Josephat (Graiyaki), Fatuma Ismail (Twibhoki, Mara), Nyamwikondo Malisa (Twibhoki, Mara) Mediana Yusuph (Twibhoki, Mara) Assia Iddy (Twibhoki, Mara) na Rahab Marwa (Twibhoki, Mara). Wengine ni Alamoki Sanga (Rweikiza, Kagera), Maria Edson (Rweikiza, Kagera, Careen Katamuru (Graiyaki, Mara) na Janeth Majula (Samandito, Geita).

**WAVULANA 10 BORA KITAIFA**

Dk. Msonde aliwataja wavulana 10 bora kitaifa kuwa ni Huma Masala (Kwema Modern, Shinyanga), Gregory Alphonce (Twibhoki, Mara), Nyambina Suma (Graiyaki, Mara), Andrew Mabula (Kwema Modern, Shinyanga) na Jonas Ayubu (Little Flower (Mara).

Wengine ni Emmanuel Paul (Kwema Modern, Shinyanga), Emanuel Marwa (Kwema Modern, Shinganya), Prosper Tumbo (God's Bridge, Mbeya), Yesaya Bendera (God's Bridge, Mbeya) na Mashana Mabao (Twibhoki, Mara).

**SHULE 10 BORA KITAIFA**

Dk. Msonde alizitaja kuwa ni God's Bridge (Mbeya), Bunazi Acres (Kagera), Twibhoki (Mara), Kwema Modern (Shinyanga), Graiyaki (Mara), Kemebos (Kagera), Rwekiza (Kagera), St. Anne Maria (Dar es Salaam), Mumtaaz (Mwanza) na Rocken Hill (Shinyanga).

**ZILIZOPANDISHA UFAULU**

Dk. Msonde ilizitaja shule 10 ambazo zimeongeza ufaulukuwa ni Mwandu Kisesa (Simiyu), Magana (Mara), Ng'hoboko (Simiyu), Tindabuligi (Simiyu), Nonwe (Shinganya), Mwashagata (Simiyu), Idoselo (Simiyu), Giyuki (Simiyu), Ipililo A (Simiyu) na Masanga (Simiyu).

**ZILIZOSHUKA UFAULU**

Alizataja kuwa ni Chororo (Mtwara), Mpanda (Tanga), Mabawe (Kagera), Mapinduzi (Singida), Ng'wabagalu (Geita), Muhuwesi (Ruvuma), Milidu (Mtwara), Mbwei (Tanga), Udutu (Tabora na Ng'ongolo (Mtwara).

**MIKOA ILIYOONGOZA**

Dk. Msonde aliitaja kuwa ni Dar es Salaam, Arusha, Simiyu, Katavi, Kilimanjaro, Iringa, Kagera, Morogoro, Pwani na Mwanza.

Mikoa mitatu iliyoongeza ufaulu kwa miaka mitatu mfululizo, Dk. Msonde aliitaja kuwa ni Simiyu, Mara na Lindi na iliyoshuka mfululizo kwa miaka mitatu ni Mtwara na Singida.

**HALMASHAURI 10 ZILIZOONGOZA**

Dk. Msonde alizitaja kuwa ni Arusha Jiji, Kinondoni, Mwanza Jiji, Hai, Moshi Manispaa, Ilemela, Bariadi Mji, Arusha, Malinyi na Mlele.

Alisema kwa upande wa halmashauri na manispaa 10 zilizoongoza ufaulu mfululizo kwa miaka mitatu ni Meatu, Butiama, Musoma vijijini, Uvinza, Itilima Vijijini, Kilosa, Chemba, Nachingwea, Bariadi Vijijini na Igunga. Kwa upande wa halmashauri na manispaa zilizoshuka ufauli mfululizo kwa miaka mitatu, alizitaja kuwa ni Nanyumbu, masasi mji, Iramba, Masasi, Kilindi, Babati vijijini, Mkalama, Newala, Mtwara vijijini, na Temeke.

# Prof. Kabudi: Hatuko tayari kudharauliwa sababu pesa

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema Tanzania haitakubali kudharauliwa na taifa lolote kwa sababu ya misaada na pesa.

Amesema Tanzania iko tayari kuwasilikiza, kujadiliana na taifa lolote ambalo linadhani kuna upungufu umejitokeza.

Alitoa kauli hiyo jana mjini Dodoma, wakati akizungumza na wafanyakazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

“Nyerere ni kiongozi barani Afrika aliyefanya mambo makubwa kuliko mwingine yoyote. Aliwafukuza watalaam wa Kijerumani na kuwarudishia fedha yao yote Deutsch Mark milioni 35.

“Kati ya pesa na heshima ya nchi yetu, tutasimamia heshima ya nchi yetu, kati ya misaada na utu wetu tutasimamia utu wetu. Hatutakubali kutoheshimiwa na utu wetu kudharauliwa kwa sababu ya misaada na pesa,” alisema na kuongeza:

“Lakini tutashirikana na mataifa yote duniani ambayo yanatuheshimu kwamba sisi ni taifa huru, pamoja na kutuheshimu sisi ni binadamu tulio sawa kama binadamu wengine.”

Prof. Kabudi pia alisema uvumi kuwa yako mataifa yanatishia kutokutoa msaada kwa Tanzania hauwezi kuliyumbisha taifa.

Siku zote, alisema Tanzania iko imara na kwa hiyo haiwezi kukubali kupewa misaada ya aina yoyote ambayo mwisho wake si mwema kwa tamaduni na mila za taifa.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, ACP Salum Hamduni, akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lenye mwili wa Naibu Kamishna wa Polisi, Dhahir Kidavashari kabla ya mazishi yake, katika kijiji cha Kwaugoro, wilayani Arumeru, mkoani humo juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wafungwa waliompora silaha askari, kumjeruhi wakamatwa

**NA FRANCIS GODWIN,** IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa limewakamata wafungwa wanne wanaodaiwa kutoroka baada ya kumshambulia kwa mapanga na kumjeruhi mwilini mlinzi, askari Magereza na kumpora silaha.

Wafungwa hao wanadaiwa kumpora bunduki aina ya Uzi-gun yenye namba TZPS 5570-062974 Sajeni Feedolin Madembwe (53) wa gereza la Iringa, mkazi wa Kibwabwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, alisema juzi kuwa tukio la wafungwa hao kutoroka lilitokea Novemba 16, mwaka huu, majira ya mchana katika msitu wa Wilolesi, Manispaa ya Iringa, wakati askari huyo akiwasimamia wafungwa kuchanja kuni kwa ajili ya matumizi ya chakula gerezani .

Aliwataja wafungwa hao waliokamatwa kuwa ni Richard Mbondamila (22) mkazi wa Imalutwa, Ilula wilayani Kilolo aliyekuwa akitumikia kifungo cha miaka mitano jela kwa kosa la wizi, Haroun Boniphace (22) mkazi wa Majengo Migoli mkoani njombe aliyekuwa akitumikia kifungo cha miezi saba kwa kosa la kujeruhi wanyama.

Wengine ni Staford Kalinga (20) mkazi wa Mtuwa Ilula, wilayani Kilolo aliyekuwa akitumikia kifungo cha kukutwa na bangi na Isack Kawogo (24) mkazi wa Mgodini, Ramadhani mkoani Njombe aliyekuwa akitumikia kifungo cha miaka minane kwa kosa la kuvunja na kuiba .

Alisema baada ya kupata taarifa za kutoroka, Jeshi la Polisi lilianza msako mkali na usiku wa Novemba 16 majira ya saa 4:00 usiku, waliwakamata Mbiondamila na Boniphace eneo la Gangilonga wakiwa katika jitihada za kutoroka kwenda Iringa mjini. Pia alisema siku ya pili walimkamata Kalinga akiwa eneo la Ndiuka akijaribu kutoroka.

Kamanda Bwire alisema usiku wa kuamkia Novemba 20, Kawogo ambaye alikuwa akifahamika kwa jina la kiuhalifu kama Mnyapara, aliyepora silaha ya askari magereza, alikamatwa akiwa Njombe na tarifa kamili itatolewa na polisi mkoani humo.

Katika hatua nyingine, Kamanda Bwire alisema jeshi hilo linajivunia mafanikio makubwa katika kesi ya ubakaji baada ya mwaka 2018 kumkamata Akwino Mtavangu (36) mfanyabiashara mkazi wa Mafinga kwa tuhuma za kubaka mtoto mwenye umri wa miaka sita, mwanafunzi wa darasa la kwanza (jina lake na shule vinahifadhiwa).

Mtavangu anadaiwa kuwa siku ya tukio, alimrubuni mtoto huyo akiwa anatoka shuleni na kumpandisha kwenye pikipiki na kwenda naye nyumbani kwake kisha kumbaka na kumficha kwenye nyumba ambayo haijaisha.

Mtuhumiwa huyo alifikishwa mahakamani na Oktoba 19, mwaka huu, katika Mahakama ya MKazi Mkoa wa Iringa, alikutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela .

# Dk. Mwinyi awatwisha zigo mawaziri



Sehemu ya mawaziri wakifuatilia hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), baada ya kuapishwa Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NI mzigo mzito. Ndivyo inavyoweza kuelezwa baada ya rais wa Zanzibar, Dk. Hussien Mwinyi, kuwapa maagizo 13 mawaziri aliowateua na kuwaapisha jana huku akionyesha hana mzaha na atakayekwenda kinyume cha hayo.

Katika hafla ya kuwaapisha iliyofanyika Ikulu, Zanzibar, Dk Mwinyi aliwataka mawaziri 13 kutekeleza maagizo 13 ambayo kwa kiasi kikubwa yanaonekana ni mzigo mkubwa kwao maana amesema atakayeshindwa kutekeleza atamwondoa.

Alisema mkataba wake na watendaji aliowateua, wakiwemo mawaziri, ni kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kikamilifu na hatasita kumwondoa yeyote atakayeshindwa kuwajibika.

Dk. Mwinyi aliwaagiza mawaziri hao kila mmoja kuhakikisha anaijua wizara yake na taasisi zilizomo katika wizara husika haraka iwezekanavyo na kuanza kazi mara moja, kutengeneza mpango kazi wenye bajeti kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), hotuba yake ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi na ahadi zake alizozitoa wakati wa kampeni.

Pia aliwataka kuwashirikisha wadau katika taasisi mbalimbali ili kupata maoni yao kwa sababu huwezi kutekeleza kazi kwa ufanisi bila ya kuwashirikisha wadau.

"Natoa mfano kama Wizara ya Elimu ina wadau wengi ambao wanaweza kutoa maoni mazuri. Washirikishe, chukua maoni ya wadau, huwezi kufanya kazi vizuri kama hujakutana na chama cha walimu. Mhakikishe kila mmoja anakutana na wadau," alisema.

Alisema dira ya maendeleo iwe kigezo cha mpango kazi wao wenye bajeti kwa sababu mpango bila ya bajeti ni rasimu isiyofaa.

### MIRADI YA WIZARA

Pia aliwataka kutembelea miradi yote iliyomo katika wizara zao na kujiridhisha na kiwango cha ubora wake, utaratibu wa zabuni uliotumika, malipo kwa makandarasi, na muda wa kukamilisha mradi husika.

"Katika hili nataka nitolee mifano kwa siku chache nilizokaa ofisini. Nilitembelea baadhi ya maeneo nimesikitishwa sana na kiwango cha miradi tunayoifanya. Mathalani nimekwenda katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tuna mradi pale wa jengo la macho, kuna jengo la kisasa la kufanya upasuaji wa macho mpaka leo halifanyi kazi sababu kuna beseni moja la madaktari kujiosha kabla ya kuingia katika upasuaji halijawekwa. Haiwezekani haya ndiyo tunayoyasema hatuwezi kukubali mambo ya namna hii.

"Nimekwenda bandarini nikaambiwa moja ya sababu ya mizigo kuchelewa kutoka ni kwamba kuna baadhi ya wafanyabiashara wanachelewa kuchukua mizigo yao, wanaifanya bandari kuwa sehemu ya kuhifadhia bidhaa zao. Nikauliza ni hatua gani mlizozichukua nikaambiwa kuwa Saateni lipo ghala la kuhifadhia mizigo nikasema twendeni lakini jengo hilo limechelewa kukamilika na mkandarasi ameshalipwa fedha zote. Iwe ni mwisho katika mambo haya," alisema.

Pia alisema juzi Makamu wa Pili wa Rais alifanya ziara katika mradi wa uzalishaji wa vifaranga vya samaki lakini hakuna uzalishaji unaofanywa, hivyo akataka apewe ripoti ya kina kuhusu mradi huo.

### UWAJIBIKAJI

Aliwataka mawaziri hao kuwa watendaji na kila mfanyakazi kuhakikisha anawajibika kwa kazi aliyopewa ili huduma zinazotolewa kwa wananchi ziwe bora na kisasa na kusiwe na malalamiko.

Dk. Mwinyi alisema kuna maeneo mengi bado huduma ni duni, watu hawawajibiki na huduma zinazotakiwa kutolewa hazitolewi, hivyo akawataka mawaziri kwenda kufanya kazi na kuhakikisha haki za watu zinatolewa.

"Mfano kuna malalamiko makubwa katika Wizara ya Ardhi, watu wananyang'anywa ardhi zao, hakikisheni mnaondoa matatizo kwa kuweka mfumo mzuri wa kukutana na wananchi kuwasikiliza shida zao. Ninataka taarifa karibu na uchaguzi kuna ardhi nyingi zimetolewa nataka orodha ya yote hayo,' alisema.

### RUSHWA NA UBADHIRIFU

Alieleza kuwa kuondoa rushwa na ubadhilifu kwa sababu kuna rushwa na ubadhilifu mkubwa unaofanywa katika upotevu wa mali za serikali.

Alisema kuna baadhi ya wizara kuna makusanyo lakini fedha hazikusanywi, kuna fedha za bajeti zinazoibiwa, kuna fedha zinazopelekwa katika miradi lakini miradi hiyo haitekelezwi hivyo kuondoa wizi katika wizara zao.

"Waziri ukishindwa kushughulikia hayo maana yake hunifai na bahati nzuri. Mkataba tuliotia saini leo (jana) hauna muda. Ukifanya vizuri utabaki na ukifanya vibaya utaondoka. Naomba tusifichane, niliwaahidi wananchi sitakuwa na huruma na muhali hivyo nitaanza na ninyi mawaziri"alisema.

### MAKUSANYO YA MAPATO

Alisema ukusanyaji wa fedha za mapato wizara zenye kukusanya mapato ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB), haufanyiki ipasavyo na kumtaka Waziri wa Fedha kuvifuatilia vyombo hivyo. Alisema fedha nyingi zinapotea na kumtaka kurekebisha hali hiyo mara moja.

### UBUNIFU, KUACHA URASIMU

Dk. Mwinyi aliwataka kuwa wabunifu kwa kubuni mbinu mpya zitakazoleta ufanisi hivyo kuwatumia wataalamu katika wizara zao kubuni njia mpya za kufanya kazi.

Alisema kuna urasimu mkubwa, hivyo hauna budi kuondolewa katika kupata huduma kwa sababu wananchi wanazungushwa katika kupata huduma mbalimbali.

"Nataka mwondokane na tatizo la urasimu katika kutoa huduma wa lile tatizo la njoo kesho liwe basi tena. Watendaji muwe tayari kujibu barua na maombi ya wananchi na sio kukaa kimya,"alisema.

"Mambo yenye maslahi ya umma yasicheleweshwe, muda wetu ni miaka mitano hatuna muda mwingine. Msikae mkasema mtafanya mwakani anzeni kufanya sasa. Toeni uamuzi kwa mambo yenye maslahi ya umma," alisema.

Sambamba na hilo, aliwataka kuwa wepesi wa kupeleka mapendekezo kubadilisha sheria kama sheria husika ni kikwazo kwa sababu kuna baadhi ya matatizo yanasababishwa na sheria zilizopo na kutolea mfano wa masuala ya udhalilishaji, hivyo kuangalia sheria zinazokidhi kukomesha vitendo hivyo.

### UTOAJI TAARIFA

Aliwataka kutoa taarifa za kazi wanazozifanya kwa waandishi wa habari hivyo kuhakikisha wanakua marafiki na waandishi wa habari hakuna haja ya kuficha wanachokifanya na kuelezea mafanikio na changamoto na si kuwakimbia waandishi.

Aliwataka kusikiliza malalamiko ya wananchi na kila wizara kuwa na utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyatafutia ufumbuzi.

### AAHIDI USIKIVU

Dk Mwinyi aliwataka mawaziri hao kuanza kazi na yuko tayari kusikiliza kikwazo chochote, hivyo kumweleza na kuchukua hatua kwa yale ambayo yapo nje ya uwezo wao katika kuchukua hatua.

Alisema amekamilisha safu ya mawaziri na kwamba matarajia ya wananchi kwao ni makubwa, hivyo wale mawaziri wazoefu waendelee kuonyesha uzoefu wao na wale wapya wakahakikishe wanaleta utendaji mpya.

"Waheshimiwa Mawaziri nakupeni hongera sana lakini wakati huo huo nawapeni pole kwa sababu mzigo niliokupeni ni mkubwa, hivyo hakikisheni mnatekeleza wajibu wenu,' alisema.

## HABARI KITAIFA

# NICOL yaahidi kuongeza gawio

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Uwekezaji ya NICOL imeahidi kuendelea kuongeza gawio kwa wanahisa wake kutokana na mipango mizuri ambayo imewekwa na uongozi ya kuwekeza kwenye miradi yenye faida.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni hiyo, Dk. Gideon Kaunda, wakati wa Mkutano Mkuu wa Kampuni hiyo uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam.

Alisema uongozi mpya wa kampuni hiyo umefanya kazi kubwa mpaka kuongeza gawio kutoka Sh. sita zilizotolewa mwaka jana kwa wanahisa wake mpaka kufikia Sh. 10 iliyotolewa mwaka huu.

Dk. Kaunda alisema anaamini mambo yataendelea kuwa mzuri kwa kuwa wamewekeza kwenye kampuni kubwa kama Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Benki ya NMB, Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE), Kampuni ya Simu ya Vodacom na kwenye viwanda vya uzalishaji wa saruji.

Uongozi wa sasa wa NICOL, alisema unapata ushirikiano mkubwa kutoka vyombo kama Mamlaka ya Masoko na Mitaji CMCA na DSE ambao wamekuwa wakiwapa miongozo na maelekezo ya namna ya kutatua changamoto wanazokumbana nazo.

Alisema kuna wawekezaji kutoka nje ya nchi kama Marekani na Australia hivyo aliwahimiza Watanzania wengi zaidi kuiunga mkono kampuni hiyo kwani inakwenda vizuri na watanufaika na uwekezaji wao.

"Wanahisa wa NICOL wanaimani kubwa na menejimenti yao na wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa sana na kwenye kura ya mapendekezo tuliyoyatoa wengi walikuwa wakiyakubali ndiyo maana yote yamepita kwa zaidi ya asilimia 90," alisema.

Alisema tangu waingie madarakani mwaka 2012 wamekuwa wakitoa gawio kwa wanahisa wao hata pale wanapopata changamoto wamekuwa wakitoa tofauti na ilivyokuwa kabla hawajaichukua.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Fedha wa NICOL, Erasto Ngamilaga, alisema kuna dalili njema za kukua kwa kampuni hiyo na kuendelea kutoa gawio zuri kwa wanahisa wake.

"Tutaendelea kuongeza kwa namna tunavyopata mafanikio kwenye uwekezaji nawaambia wanahisa NICOL wajivunie kuwa kwenye kampuni yenye mwelekeo sahihi nawaomba ambao hawajanunua hisa waje kununua," alisema.

**Tangu waingie madarakani mwaka 2012 wamekuwa wakitoa gawio kwa wanahisa wao hata pale wanapopata changamoto wamekuwa wakitoa tofauti na ilivyokuwa kabla hawajaichukua.**

# Ndugai awapa kazi wabunge haki za watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wabunge kusoma na kuzielewa ajenda za watoto na vijana ili kuisaidia serikali kutekeleza malengo endelevu ya maendeleo (SDG).

Ndugai aliyasema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto Duniani yaliyofanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa, bungeni jijini hapa.

Alisema wabunge wanatakiwa kusoma kitabu cha ajenda za watoto na vijana kilichotolewa na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) ili kuzielewa na kuisaidia serikali kutekeleza masuala mbalimbali ambayo imetia saini katika mikataba ya kimataifa.

"Bunge letu tukufu tayari lilishaingia makubaliano na shirika linalojihusisha na masuala ya watoto duniani (UNICEF) katika kusaidia kupambania haki za watoto," alisema Ndugai.

Aidha, alisema Bunge lake liko tayari kufanya kazi na mashirika mbalimbali nchini na yale ya kimataifa ili kusaidia kulinda haki za watoto na vijana.

"Niwakaribishe sana ndugu zangu wa UNICEF hapa bungeni na niwaahidi kuwa Bunge tuko tayari kufanya kazi na nyinyi na tunashukuru maadhimisho ya Siku ya Mtoto Duniani mwaka huu kuyafanyika hapa bungeni kwa kuwapa fursa wabunge ambao asilimia kubwa ni wapya kutambua umuhimu wa kulinda haki za watoto, alisema Ndugai.

Pia alitoa wito kwa UNICEF kutoa elimu kwa wabunge kwa njia ya semina, mafunzo pamoja ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kujifunza mambo yanayohusu haki ya mtoto.

Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa (UN) nchini, Zlatan Milisic, alisema anaipongeza serikali ya Tanzania kwa jitihada inazozifanya ili kulinda haki za mtoto.

Alisema maadhimisho ya Siku ya Mtoto Duniani mwaka huu yanafanyika ikiwa imepita miaka 31, tangu mkataba wa kimataifa kuhusu kulinda haki za mtoto utiwe saini.

Aidha, Mwakilishi wa UNICEF, Shalini Bahuguna, alisema bado kero mbalimbali zinazowakabili watoto katika jamii ambazo serikali inatakiwa kuwekeza jitihada zaidi ili kuzitatua.

Bahuguna alisema kuwa serikali ya Tanzania inatakiwa kuendelea kuwekeza kwa watoto ili kusaidia kuwaondolea kero mbalimbali ambazo zinachangia kukwamisha ndoto zao.

Awali, mtoto kutoka Mbeya, Agape Joster (13), aliwaeleza wabunge kuwa wanakabiliwa na kero mbalimbali hasa ukosefu wa mabweni kwa wanafunzi wa shule za kata hali inayosababisha wengi wao kupata mimba.

Alisema, watoto wa kike pia wamekuwa wakikabiliana na tatizo za unyanyasaji wa kijinsia katika jamii zao hali inayochangia wengi wao kushindwa kutimiza ndoto zao za kupata elimu.

Abdulltif Hassan (16) kutoka Shule ya Sekondari Chuini, Zanzibar, alisema wanaiomba serikali kuwasaidia kutafuta namna bora itakayo wasaidia kuwa na madawati ya kutoa malalamiko ya kufanyiwa unyanyasaji wa kijinsia.

"Hivi sasa kuna madawati ya kijinsia lakini mengi yapo katika vituo vya polisi hali ambayo inatia ugumu kwa watoto kwenda polisi kutoa malalamiko yao hivyo tunaiomba serikali itusaidie kutafuta namna nyingine ya kutusaidia"alieleza Hassan



Meneja Uzalishaji wa kiwanda cha kuunganisha na kutengeneza magari cha GF Vehicle Assemblers Ltd (GFA), Laban Dundo (kulia), akifafanua jambo kwa wafanyakazi wa kampuni ya GF Tucks & Equipment Ltd, walipotembelea kiwandani hapo, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Afungwa miaka mitano kwa kuvunja, kuiba mali za shule

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Mtaa wa Serengeti, Tarime mkoani Mara, Francis Mokera, amehukumiwa kifungo cha miaka mitano jela baada ya kupatikana na hatia ya kuvunja na kuiba mali za shule.

Mokera alihukumiwa juzi katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime baada ya kukutwa na hatia ya kufanya kosa hilo na kuiba magodoro, viti na taa za umeme, mali za Shule ya Sekondari Tarime zenye thamani ya Sh. 2,850,000.

Akisoma Hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Vincensia Balyahula, alisema ameridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka bila kuacha shaka.

Awali, Mwendesha Mashitaka Thabiti Temba alidai mahakamani hapo kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo baada ya kuvunja milango ya shule na kuiba vitu hivyo kati ya Machi na Mei, mwaka huu, hivyo kusababisha hasara kwa shule hiyo na wanafunzi kuathirika katika masomo yao.

Hakimu Balyahula alisema: "Vitendo hivyo ni hujuma kubwa kwa wanafunzi, hivyo mahakama hii inakuhukumu kwenda kutumikia kifungo cha miaka mitano jela ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaohujumu mali za umma na kuwarudisha wanafunzi nyuma kielimu."

Baada ya hukumu hiyo, walimu wa shule hiyo waliokuwa nje ya mahakama, walisikika wakisema haki imetendeka.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Juhudi za makusudi zinatakiwa mapambano dhidi ya UKIMWI*

**SERIKALI** imetoa takwimu mpya zinazoonyesha maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU) kuwa wastani wa watu wanane kwa siku wanapata maambukizi hayo, sawa na watu 72,000 kwa mwaka.

Katika taarifa hiyo, iliyotolewa juzi na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, kuelekeza Wiki ya Kilele cha Siku ya UKIMWI Duniani itakayofanyika Desemba Mosi ambayo kitaifa yatafanyika mwaka huu Moshi, mkoani Kilimanjaro, alisema vijana ndilo kundi lililoko katika hatari zaidi.

Mwaluko alibainisha kuwa hali hiyo inatokana na ongezeko kubwa la maambukizi kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 15 mpaka 35 na kwamba hatua hiyo, inachangia maambukizi mapya kwa zaidi ya asilimia 50.

Takwimu hizo, licha ya kuonekana kama si tishio, kwa mtazamo wa juu juu, ni hatari kwa mustakabali wa ustawi wa nchi kwa kuwa waathirika wakubwa ni vijana ambao ni tegemeo kubwa kwa nguvu kazi ya taifa.

Huo ni ukweli kwa sababu wakati Tanzania ikitekeleza mpango wa maendeleo ya uchumi wa kati ambao dhima kuu ni mapinduzi ya viwanda, kama hatua madhubuti hazitachukuliwa katika kuokoa kundi hilo, ndoto za kufikia azma hiyo zinaweza kugonga mwamba.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba maendeleo yoyote ya kijamii na kiuchumi katika jamii yoyote yanategemea kwa kaasi kikubwa afya za wananchi. Tunasema hivyo kwa sababu kama idadi kubwa ya wazalishaji hawatakuwa na afya njema, ni wazi kwamba uzalishaji utadorora na matokeo yake hakuna maendeleo.

Kutokana na ukweli huo, jitihada za makusudi zinapaswa kuchukuliwa na kila mwananchi, serikali, sekta binafsi kuhakikisha mipango na mikakati iliyowekwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI inatekelezwa.

Mwaluko aliweka bayana katika taarifa yake kwamba serikali inatekeleza mikakati katika kuzuia maambukizi mapya kwa wale ambao bado hawajaambukizwa na wale ambao tayari, kuhakikisha wanapatiwa dawa za kufubaza VVU (ARV).

Mkakati huo, kwa mtazamo yakinifu unaonyesha wazi kwamba serikali imejipanga kwa vitendo katika kufikia malengo yake kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI, hivyo ni jukumu la wadau kushiriki na kuhakikisha kunakuwa na mafanikio makubwa.


Pamoja na mikakati iliyowekwa na serikali, ni vyema pia nguvu zaidi ikaelekezwa katika shule za sekondari, taasisi za elimu ya juu na makundi maalum ambako kuna vijana wengi na ndio walio katika hatari ya kupata maambukizi.

Katika taasisi za elimu ya juu, kwa mfano, wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa shahada ya kwanza wanatarajiwa kuanza masomo hivi karibuni na wengine kuendelea wa mwaka wa pili hata wa tatu. Huo ni wakati mwafaka wa kupewa elimu juu ya kujikinga na maambukizi ya VVU.

Wanafunzi hao liwe kundi lengwa namba moja kwa sababu ushahidi wa wazi unaonyesha kwamba wamekuwa huru kupita kiasi, hivyo ni rahisi kukumbwa na tatizo hilo. Nyakati za wikiendi na usiku, mathalan, wengi wao wamekuwa wakiranda randa katika majumba na kumbi za starehe hali ambayo inaonyesha dhahiri kwamba wanakuwa katika hatari ya kupata virusi.

Kila mtu anapaswa kuwajibika kwa nafasi yake kuhakikisha taifa linakuwa salama dhidi ya UKIMWI ili kufikia ndoto za serikali za kufikia uchumi wa kati na pia kuokoa kizazi cha sasa na cha baadaye.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# *Haya yakizingatiwa hakuna migogoro hii katika familia*

**KATIKA** miaka ya hivi karibuni kumekuwapo na matukio ya wajane kupoteza haki zao baada ya waume zao kufariki dunia bila kuacha wosia, tatizo ambalo haliishii kwao tu, bali hawakumba hata watoto.

Matatizo hayo yanatokana aidha kwa kutojua ama kwa kujua, lakini hakuna anayeona umuhimu wa kuandika wosia. Hali hiyo wakati mwingine inasababisha migogoro kwenye baadhi ya familia hadi kutokea maafa katika baadhi ya familia.

Wakati hayo yakiendelea katika jamii, serikali kwa kushirikiana na taasisi zake na wadau mbalimbali imekuwa ikijitahidi kutoa elimu ili kuhakikisha kila Mtanzania anaelewa umuhimu wa kuandika wosia au kuacha wosia.

Mfano mmojawapo ni hivi karibuni Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Dovetha Kamuzora, alitoa elimu hiyo kwa baadhi ya wakazi wa jijini Dar es Salaam na kusisitiza pia uteuzi wa wasimamizi wa mirathi wanaoaminika.

Naibu msajili huyo ambaye aliakwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kutoa elimu hiyo, alisema baadhi ya watu hawaandiki wosia kwa kuwa wanaamini kufanya hivyo ni uchuro, hivyo hawaoni sababu.

Kwa hayo yanayosemwa na naibu msajili huyo, ni vyema sasa Watanzania wakabadilika na kuzingatia na kuandika wosia ili wanapofariki dunia, wasiache migogoro nyuma inayosambaratisha familia zao.

Ni kweli kwamba, kila binadamu yuko safarini kuelekea kifo, hivyo ni vyema kujiandaa wakati wa uhai wake ili akifa waliokuwa wakimtegea wabaki wakiwa salama.

Wosia na mirathi ni mambo muhimu katika kufanikisha usimamizi wa mali za marehemu, lakini kuwapo msimamizi wa mirathi mwaminifu asiyefuja mali za marehemu ni jambo la msingi.

Maana yake ni kwamba marehemu asipoacha wosia, anaibua migogoro na hata kama ameacha wosia, akiteuliwa msimamizi wa mirathi asiye mwaminifu, bado anazusha migogoro katika familia.

Hivyo, kuzingatia mambo hayo mawili, ni muhimu zaidi ili kuepusha migogoro ambayo wakati mwingine husababishwa na marehemu kwa kutoacha wosia ama familia yenyewe kwa kutoteua msimamizi mwaminifu wa mirathi.

Taratibu za uandishi wa wosia ziko wazi kwamba ule wa maandishi unatakiwa kushuhudiwa na watu wawili pale huku mtoa wosia mwenyewe akiwa na akili timamu na anajua kusoma na kuandika.

Mmoja wa mashahidi awe ni ndugu wa karibu wa mtoa wosia, wa pili si lazima awe ndugu wa karibu, na wosia unatakiwa uwe na tarehe, uandikwe kwa karamu ya wino na kuwekwa saini ya mtoa wosia wa mashahidi.

Kwa mtoa wosia asiyejua kusoma na kuandika, anatakiwa kuwa mashuhuda wanne wanaojua kusoma na kuandika, na ataweka saini ya kidole gumba cha mkono wa kulia, mashuhuda na washuhudie na kutia saini.

Lakini pia kuna wasia wa mdomo, ambao unatakiwa kuwa mashahidi nne, wawili kati yao wawe ni ndugu wa mtoa wosia na wengine wasio ndugu wa mtoa wosia, ingawa unaweza usitumike.

Wosia wa maandishi haubadilishwi na wosia wa mdomo, ila wa mdomo unaweza kubadilishwa na wa maandishi na mtoa wosia ana haki ya kuandika ama kutaja sehemu tu ya mali zake katika wosia wake.

Mali ambazo hazijaandikwa zitasimamiwa kwa utaratibu wa mirathi, na pia mtu aliyetimiza umri uliokubalika kisheria, miaka 21, ndiye anayeweza kuandika wosia na awe mwenye akili timamu.

Hata hivyo, wosia unaweza kukataliwa iwapo itagundulika kuwa wakati mhusika anaandika, akili yake haikuwa sawa ama kutokana na ukichaa, ugonjwa, ulevi au sababu nyingine.

Kwenye suala la utunzaji wa wosia, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umeweka wazi jinsi ambavyo mtu anaweza kuandika na kwenda kuutunza huko kwa ajili ya usalama zaidi.

Ikumbukwe kuwa RITA ni chombo cha serikali chenye dhamana ya kusimamia mirathi, na utunzaji wa wosia ni moja ya majukumu yake, hivyo kama mwandikaji ataona hana pa kutunzia nyumbani awape wamtunzie.

Msisitizo upo katika kuwapo kwa wosia na pia msimamizi mwaminifu wa mirathi ili kuepusha migogoro, ambayo huwa inaibuka wakati mtu anapofariki ama wakati wa usimamizi wa mali za marehemu.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Bunge letu tukufu lisigeuzwe kijiwe cha matusi, vijembe

AKIFUNGUA Bunge la 12, Rais John Magufuli, alisema kuwa angependa kukosolewa kwa hoja na kutoa suluhu, yaani ukosoaji chanya na wa kujenga (constructive criticism). Kwa msingi huo, safu hii itaitikia wito wa rais kwa kutoa ukosoaji chanya kuhusiana na kituko kilichoshuhudiwa bungeni hivi karibuni kwenye ufunguzi wa bunge tajwa ambacho si rahisi kuvumilia kuogopa kuweka mfano (precendent) mbaya. Katika muda huu tajwa, mbunge mmoja mpya ambaye safu hii inamheshimu na kumhusudu sana aliwaacha wengi vinywa wazi. Kwani, mhusika pamoja na uanagezi wake alipewa fursa ya kuongea kwa niaba ya wabunge wakati ilikuwa ni mara yake ya kwanza kuongea bungeni. Hapa nadhani ndipo kosa lilianzia. Unampaje nafasi mwanagezi kuongea wakati kuna wakongwe ambao wameyazoea mawimbi kama haya? Mbunge huyu bila woga wala tahadhari, alitamka maneno yenye ukakasi tena mbele ya rais huku akishangiliwa kwa mshangao wa wengi wakati mhusika akizidi kukoleza. Katika fursa hii ya kuongea bungeni, mhusika bila kuzingatia kuwa kila kinachoongelewa kinatunzwa alimkariri Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza, Sir Winston Churchill, akisema kuwa kama unakwenda mahali na njiani mbwa wakawa wanakubwekea, ukiamua kumtupia au kuwatupia mawe kila mbwa wanaobweka, hutafika. Pia Churchill aliwahi kusema kuwa ni jambo jema mtu asiye msomi kusoma vitabu vya nukuu. Hapa muhimu ni kuzitumia vizuri. Je, kwa kuwashambulia wahusika kwa kuwalinganisha binadamu na mbwa siyo kuanza kuwatupia mawe hao mbwa husika? Mbunge huyu mwanagezi alimaanisha wapinzani wanaolalamikia matokeo ya uchaguzi ambayo ni haki yao ilimradi madai yao yawe na mashiko.

Watanzania ni ndugu na tunaheshimiana tukishindana kwa hoja na si mapanga. Hakuna haja ya bunge letu kugeuzwa kijiwe cha uhuni na matusi. Hakuna Mtanzania anayeweza kulinganishwa na mbwa hata awe hakubaliani nasi. Unapowaita wapinzani mbwa unakaribisha yafuatayo:

Mosi, unawapa fursa wakujibu kwa kukutukana wewe na hata taasisi matusi mengi mazito bila sababu. Kwanini kulinganisha Watanzania na mbwa wakati kama ni misemo ya busara ya kukaripia kadhia hii ipo tena mingi? Mfano, msemaji angesema kuwa kelele za mpangaji hazimnyimi usingizi mwenye nyumba. Tuwe na bunge la kistaarabu kama ambavyo ilikuwa kwenye kampeni; na si la matusi na visasi.

Pili, kuwaita wapinzani mbwa maana yake ni kuwaita Watanzania wote mbwa. Kwani, wapinzani nao ni Watanzania sawa na wengine. Wanaweza kukosa, kukosea na mengine kama hayo. Lakini bado hakuna mwenye haki ya kuwaita au kuwalinganisha na mbwa. Hivi nao wakiamua kukuita wewe na wenzio mbwa utafurahi na kuvumilia? Usiishi kwenye nyumba ya vioo ukawatukana watupa mawe.

Tatu, kwa kuwaita wapinzani mbwa, msemaji alipaswa ajue anamaanisha kuwa walishindana na kuwashinda mbwa jambo ambalo haliingii akilini. Kwani, mbwa hawezi kushindana na binadamu bali mbwa wenzake.

Nne, kutolea matusi bungeni ni kuliondolea heshima na utukufu wake kama linavyoitwa siku zote. Bunge tukufu haliwezi kuruhusu matusi iwe kwa makusudi au bahati mbaya. Hivyo, ni vizuri wakubwa wa taasisi hii muhimu wakawaonya wanagezi wasiojua lugha za kutumia kwenye chombo muhimu kama hiki. Isitoshe, mbunge anayewawakilisha kweli wananchi, hajatumwa kutukana wenzake. Watu wa namna hii wanaoshindwa kuona madhara ya maneno na matendo yao, hawalisaidii taifa wala hawawatendei haki wale wanaowawakilisha ama hawajui wajibu wao na ukubwa wa jukumu la uwakilishaji wananchi.

Je, nini kifanyike? Tunashauri yafuatayo:

Mosi, kuna haja ya bunge kutoa waraka maalum kwa wabunge hasa wale wageni bungeni juu ya lugha na mienendo inayotakiwa bungeni.

Pili, inapotokea mbunge kama huyu akapotoka na kuropa, basi Spika au mkuu yeyote wa chombo husika amkaripia au kumpa adhabu mhusika papo hapo au baada ya kupata taarifa au malalamiko bila kujali yanatoka kwa nani. Katiba ya Tanzania iko wazi juu ya hadhi na nafasi ya binadamu kuwa wote tupo sawa mbele ya katiba na sheria.

Hivyo, yeyote anayedhamiria kutukana, kwanza ajiulize yeye ni nani na anayemtukana ni nani? Wajibu wa kulinda heshima ya Watanzania na taifa ni wa kila Mtanzania. Kwani katiba yetu iko wazi kuwa binadamu wote ni sawa na kila mtu anastahili heshima na ulinzi toka katika jamii.

Tumalizie tulipoanzia. Hakuna haja ya kukaribisha vituko kwenye bunge, taasisi ambayo si tukufu tu bali ni muhimu kama mmojawapo wa mhimili wa taifa. Tuonane wiki ijayo.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa

# Bunge hili tutarudi enzi za G55?

WATANZANIA mliokuwa na akili sawasawa katika miaka ya mwishoni mwa themanini na ya mwanzoni mwa tisini, mnakumbuka majina ya wabunge hawa? Njelu Kasaka, Lumuli Kasyupa, Mateo Qaresi, Jared Gachocha, Jenerali Ulimwengu, Arcado Ntagazwa, Philip Marmo na Sebastian Kinyondo (Mzee wa mitemba).

Mnawakumbuka Pahares Kabuye, Mathias Kihaule, Edward Ayila, Evarist Mwanansao, Nassoro Malocho, Guntram Itatiro, Thabita Siwale, Edith Mnuo, Dk Maria Kamm, Chediel Mgonja, Charles Kinuno na Kapteni Theodos Kasapira?

Wako 55, nikisema niwataje wote, mtaishia kusoma majina tu msipate nachotaka kusema hapa. Hao ni baadhi ya waheshimiwa walioibuka na kudai Serikali ya Tanganyika, wakijulikana kama G55.

Walitingisha hao balaa. Hebu fikiria tena walikuwa wa chama kimoja, Chama Cha Mapinduzi (CCM), hikihiki kinachoongozwa na Dk John Magufuli akisaidiwa na Philip Mangula, Dk Mohamed Sheni na Dk Bashiru Ali.

Chini ya marehemu Kasaka aliyekuwa mbunge wa Lupa, walichachamaa ile mbaya, Tanganyika ikawa Tanganyika, piga ua lazima Tanganyika irejee. Wakubwa wakasugua vichwa, kina Julius Nyerere na Ali Hassan Mwinyi.

Hatimaye upepo ukapita, mambo yakarejea mwake. Tanzania ikanusurika, Tanganyika ikaachwa iendelee kulala usingizi wa pono. Lakini hali ilivyokuwa ilibaki kiduuchu watu kugawana mbao. Tanganyika ubao wake, Zanzibar ubao wake na jahazi kuzama.

Hiyo ilikuwa kabla ya mwaka 1992, Tanzania iliporejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa. Bungeni kulikuwa na Spika gwiji Pius Msekwa. Aling'ang'ania tanga lisishushwe likapandishwa lingine, mpaka hali ikawa shwari, jahazi likasonga mbele.

Tuwapongeze waliozuia upepo huo, kwa sababu leo tungekuwa tunazungumza mengine, pengine Zanzibar leo ingekua ni nchi jirani. Amini usiamini, wabunge wa chama kimoja wakaamua kusigana kila kundi likivutia ngozi kwake.

Kumbukizi hii inanipeleka katika Bunge la 12, ambalo lilizinduliwa na Rais John Magufuli Novemba 13 mwaka huu, Dodoma. Bunge lenye wabunge karibu wote wa CCM.

Bunge ambalo baadhi ya watu kwa sababu zao, wamelipongeza kwamba sasa halitakuwa la 'matusi' na 'kejeli'. Bunge ambalo upepo unaonesha litakuwa mbashara kuliko la 11, ambalo litakuwa la faragha zaidi.

Hivi karibuni nikamsikia Spika wake Job Ndugai, akiwataka wabunge kuacha ububu na kujipendekeza, bali wafunguke na kuikaba Serikali kisawasawa ili kuwajibika kwa wapiga kura wao.

Lakini wengine kwa sababu zao, wanaponda kuwa litakuwa la Ndiyo Mzee, yaani litakuwa kibogoyo, kwa wabunge wa CCM kushindwa kuibana na kuikabili kisawasawa serikali ya CCM, kwa kuchelea kuonekana wasaliti.

Kama hatutarajii Bunge la kina Freeman Mbowe, Joseph Mbilinyi, Peter Msigwa, Godbless Lema, Tundu Lissu, Esther Bulaya, Esther Matiko, John Heche na Halima Mdee, tutarajie la aina gani?

Tutarajie la Saasisha Mafue, Tulia Ackson, Jesca Msambatavangu, Mrisho Gambo, Mwita Waitara, Robert Maboto, Michael Kembaki na Josephat Gwajima, kuwa kama lile la kina Lumuli Kasyupa, William Mpiluka, Patrick Qorro, Japhet Sichona, Mbwete Hombee, Kisyeri Chambiri, Ndembela Ngunangwa, Adam Karumbeta, Paschal Degera na Benedict Losurutia?

Yaani Bunge la chama kimoja, ambamo wanachama hicho, watasimama kidete kukabiliana na Serikali yao mpaka kieleweke. Kuna faidia ya kuwa hivi, kwamba sasa ukweli ni ukweli tu, na utaanikwa na kuaminika.

Enzi za Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, CCM walijihami dhidi ya mashambulizi ya wapinzani walioonekana kuibua mambo, na kuna nyakati kura zilipigwa CCM wakashinda kwa wingi na si kwa hoja.

Lakini sasa hakuna kuzua, nyeupe ni nyeupe na nyeusi itakuwa nyeusi mpaka majibu mwafaka yatoke, kwa sababu wanatoka nyumba moja na wanajua yaliyomo yamo. Wote wanawajua kunguni katika kitanda chao hakuna kudanganyana.

Kwa sasa hoja ikitolewa na kura kupigwa, hakutakuwa na unafiki, wanajuana kiundani na wanaijua CCM inataka nini na ni wapi inaweza kuiangusha Serikali yake.

Ndiyo sababu akiwaonya wabunge dhidi ya utoro, Spika Ndugai aliwaambia kuwa mahali pa kuwashitaki sasa panajulikana. Ofisini kwa aliyewapitisha kugombea ubunge! Tunasubiri kujionea mambo Februari. Alamsiki!

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Upotoshwaji kwenye mitandao ya kijamii ni janga kwa taifa



Na Thobias Mwanakatwe

MITANDAO ya kijamii ni huduma muhimu katika kuwasilisha ujumbe na umekuwa kiungo muhimu katika upashanaji wa habari duniani katika zama za sasa za sayansi na teknolojia.

Huduma ya mitandao ya kijamii inaweza kuunganisha watu wenye shauku/mapenzi ya aina moja (kama vile mpira wa miguu, shule, ndondi, vyakula vya aina mbalimbali, filamu, dini na urafiki. Pia mitandao ya kijamii inatumika kuwaleta watu pamoja na kujenga urafiki na kupeana taarifa na watu wengine.

Wakati wa uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu nchini, kulizuka malalamiko mengi kutoka kwa baadhi ya wananchi kutokana na mawasiliano ya mitandao ya kijamii kutopatikana. Malalamiko na shutuma zilielekezwa kwa serikali ingawa hakuna mamlaka yoyote iliyojitokeza hadharani kuelezea nini kimetokea kwenye mitandao ya kijamii.

Pia wako watu ambao walipongeza kuminywa kwa mitandao ya kijamii wakieleza kwamba uzushi kwenye mitandao hiyo ulikuwa wa kiwango cha juu hali ambayo ilikuwa hatari kwa usalama wa nchi.

Baadhi ya watu, wakiwamo wanasiasa, kipindi cha uchaguzi walitumia mitandao ya kijamii kuleta uchochezi na kupandikiza chuki kwa wananchi jambo ambalo halikuwa na afya kwa taifa.

Naungana na wale watu waliosifu uamuzi wa kuiminya mitandao ya kijamii kipindi cha uchaguzi kwa sababu ilikuwa inatumika vibaya kuleta uchochezi kwa kuandika mambo yasiyo na ukweli.

Nilidhani baada ya kusota kwa takribani wiki kadhaa bila kuwa na mitandao ya kijamii, basi wapotoshaji wangejifunza na kuanza kuitumia mitandao ya kijamii vizuri lakini naona bado dawa haikuwaingia na badala yake upotoshaji umeendelea kama kawaida.

Mfano Novemba 19, mwaka huu, kulizagaa mitandaoni kwa taarifa ya kwamba Bunge la Ulaya limeazimia kwa kauli moja kuifutia Tanzania misaada na mikopo yote ambayo imeomba kwenye Umoja wa Ulaya (EU) na washirika wake ikiwamo msaada mkubwa wenye thamani ya Sh. trilioni 1.6.

Baada ya kuzuka kwa taarifa hizo, Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji na mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Ulaya, Jestas Nyamanga, aliibuka na kukanusha vikali habari hiyo na kusema si ya kweli ni upotoshaji mtupu.

Balozi Nyamanga alisema habari hiyo ni ya uongo kwa kuwa hakuna azimio wala maazimio yoyote yaliyotolewa au kupitishwa na Bunge la Ulaya kutaka kuisitishia Tanzania misaada au mikopo yoyote inayotoka kwenye umoja kwa Tanzania au ambayo Tanzania iliomba.

Nyamanga anasema si kweli kwamba Bunge la Ulaya lilikutana badala yake kilichofanyika ni kikao tu cha Kamati ya Mambo ya nje ya Bunge hilo na kupitia kikao chake hicho cha kawaida moja ya suala lililojadiliwa katika kamati hiyo ilihusu Tanzania kama mbia wake mkubwa wa maendeleo na uchaguzi mkuu wake uliofanyika hivi karibuni. Huo ni utaratibu wa kawaida kabisa kwa bunge hilo kuweka majadiliano pindi tu nchi mbia nayo inapotoka kwenye uchaguzi mkuu.

Taarifa kwamba Tanzania imesitishiwa misaada na eti pia imezuiwa kufanya biashara na nchi yoyote ya Ulaya, Balozi anasema ni za uongo mtupu na ni upotoshaji mkubwa.

Bunge lote la Umoja wa Ulaya lina wabunge 705 na wanaotoa maoni yao ni watano tu na wala hakuna azimio, makubaliano wala chochote kilichowekwa kwa hiyo taarifa zinazoenezwa si za kweli na zinafanywa na watu wasiolitakia mema na wenye nia mbaya na taifa la Tanzania.

Kutokana na hali hiyo, Balozi Nyamanga anawataka Watanzania wapuuze taarifa hizo zinazoenezwa na watu wachache wasioitakia mema Tanzania na kwamba uhusiano wa Tanzania na Umoja wa Ulaya ni mzuri na umedumu kwa zaidi ya miaka 45 toka mwaka 1975.

Upotoshaji wa namna hii kwa nchi haukubaliki, hivyo ni lazima vyombo husika vichukue hatua ili kukomesha tabia hii ambayo inazidi kuleta mkanganyiko kwa nchi. Wanaopotosha mambo kama hayo ndio walikuwa wa kwanza kutoa lawama kwa serikali hatua ilipochukuliwa kuminya mitandao. Ifike wakati Watanzania tuwe wazalendo kwa nchi yetu tuachane na uvibaraka kwa mabeberu.

Baadhi ya nchi za Afrika ambazo zimeingia katika machafuko zilianza mambo kama hayo kwa baadhi yao kuwa vibaraka wa mataifa ya nje kwa kuibua mambo yasiyo ya kweli. Hatua zinapaswa kuchukuliwa kwa sababu hali kama hii itaendelea, ni bora mitandao ya kijamii iendelee kuminywa kama ilivyokuwa kipindi cha uchaguzi.

***MUNGU IBARIKI TANZANIA***

***Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

## DARASA LA NDOA

# Kuacha, kuambatana na kuwa mwili mmoja- 2



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka 0744000066

WATU wawili wanapooana, katika ndoa ya Kikristo imekuwa ikielezwa kuwa wanakuwa si wawili tena bali mwili mmoja. Maandiko matakatifu yanasema watawaacha baba na mama zao na kuungana na wenzi wao, hivyo muungano huo ndio unaowafanya kuwa mwili mmoja.

Kuacha wazazi haimaanishi kutelekeza au kuondoa nafasi ya wazazi kwa watoto wao, bali kutoa uhuru kwa watoto wao walioona kuendesha maisha yao ya ndoa bila kuingiliwa wala kupokea amri kutoka kwa wazazi. Kufanya hivyo ni sehemu ya kuheshimu mipaka na ndoa ya watoto wao na kutambua kuwa sasa ni watu wazima wenye uwezo wa kufanya uamuzi wao.

Hata hivyo, wazazi wanaweza kutoa ushauri pale unapohitajika na si kutoa amri. Kama ushauri unakusudia kujenga na kuimarisha maisha ya ndoa ya watoto wao badala ya kuwavuruga, unaweza kupokewa.

Wanandoa kwa kuwa ni watu wazima, wanao wajibu wa kupima kila ushauri unaotolewa au maneno wanayoelezwa na mtu yeyote yule, kwani wakati mwingine ndoa huvurugwa na ndugu, wazazi, marafiki, majirani, wafanyakazi wenzetu, yamkini hata wale tunaoabudu pamoja nao. Mara nyingi watu wanaoweza kukuumiza huwa hawatoki mbali bali ni wale walio karibu nawe. Kuna wazazi ambao hawako tayari kukubali kuwa mamlaka yao kwa watoto si ya milele. Hufikia mahali ambapo mamlaka hayo yanakuwa na mipaka. Kuna hatua katika maisha ni lazima mtoto atakuwa na haki ya kuamua juu ya maisha yake.

Kwa hiyo, wazazi wanapokuwa waamuzi wa kila jambo linalowahusu watoto wao pale wanapokuwa wameoa au kuolewa, husababisha migogoro katika ndoa za watoto wao.

Wazazi wengine wamekuwa waamuzi wa maisha ya watoto wao katika ndoa. Mzazi anaweza hata kumpangia mwanawe ampe fedha kiasi fulani kila mwezi kwa sababu tu yeye ni mzazi. Mzazi anaweza kumpangia mtoto aishi vipi na mkewe au mumewe, awalee vipi watoto wake na masuala mengine ya kimaisha. Hapa siyo tu kwamba, wazazi hawa wanaweza kwa kadiri wawezavyo kuwaingilia watoto wao kwenye ndoa zao, bali huwafanya watoto wao kushindwa kukua. Wanandoa wanawekwa katika hali ya kuamini kwamba, mzazi ndiye mwenye haki ya kumsemea kuhusu maisha yake kuliko haki yake mwanandoa mwenyewe.

Wanandoa wasioruhusiwa kukua, huwa hawako tayari kwenda kinyume cha utashi wa wazazi au ndugu, hata kama wanauona utashi huo ni kinyume na matakwa yao. Hawaamini kamwe kwamba wana haki ya kuamua kuhusu maisha yao kama binadamu kamili.

Kwa bahati mbaya nao wanaweza kuja kuwatendea watoto wao hivyo na watoto hao wakaishi bila kukua kwenye uhusiano. Ndipo unapojengwa ukoo wa wazazi au ndugu wenye kuingilia ndoa.

Wazazi au ndugu kuwa katika umaskini kimapato, kunaweza kuwa na utegemezi kwa mtoto wao. Kama tujuavyo, mtu anapooa huanza kuelekeza nguvu nyingi kwenye ndoa au familia yake, badala ya nyumbani. Kutokana na hali hiyo, ndugu au wazazi wa mume wanaweza kudhani kwamba, mke wa mtoto wao au ndugu yao ndiye chanzo cha misaada kupungua au kusimama. Umakini na kujitambua kunahitajika sana katika mambo haya.

Katika ndoa kuna kuambatana. Kuambatana maana yake kushikamana au kung'ang'aniana. Kuambatana na mke inamaanisha kuwa, mwanamume ana utambulisho mpya ambao ni uhusiano na mkewe na sio wazazi wake. Hii maana yake ni kuwa mume awe na uhusiano mkubwa na wa karibu zaidi na mkewe kuliko watu wote wengine.

Vivyo hivyo, mke inampasa kuhusiana na mume wake zaidi kuliko watu wote wengine. Hii ndiyo kusema kwamba, kwa mume, mtu wa kwanza wa kuhusiana naye, wa kumpenda na kumthamini (baada ya Mungu) awe ni mkewe, na mke vivyo hivyo kwa mumewe. Baada ya Mungu, mke au mume apate nafasi ya kwanza kabisa na ya maana katika moyo wa mwenzi wake.

Katika ndoa, wanandoa wanakuwa mwili mmoja. Hii ni zaidi ya tendo la ndoa. Maneno "kuwa mwili mmoja" yanamaanisha kina cha uhusiano wa mume na mke katika ndoa. Mwili ni sawa na mtu. Kuwa mwili mmoja kunamaanisha kuwa mume na mke wana uhusiano wa pekee kati yao. Ni watu wanaotegemeana. Mwenzi anakuwa sehemu ya nafsi ya mwenzake.

Kwa maneno mengine, wanaungana kiroho, kiakili, kimwili, kihisia, kimapato, na mambo mengine. Mke anatimiza kilichopungua kwa mumewe, kama jinsi sifa za mke zinavyokamilisha zile za mume.

Katika ndoa ambayo mume na mke wameunganika kwa namna hii, ni sawa kwamba mtu mpya kamili ameumbwa. Kila mmoja anakuwa sehemu ya mwenzake na wanafanya kila kitu pamoja kwa umoja. Wanashirikiana na kila kitu walichonacho kinakuwa ni kwa ajili ya wote.

Kabla ya ndoa, kila mmoja alikuwa akifikiri na kutenda binafsi lakini baada ya kuoana, mambo yote, ikiwa ni pamoja na yale yanayohusu kutoa misaada kwa wazazi, ndugu na watu wengine, yanapaswa kufanywa kwa kushirikiana, kushauriana na kukubaliana.

Katika ndoa hao wawili wameunganika, na neno "mimi" linachukua maana nyingine na kumaanisha "pamoja na mwenzi wangu". Kuwa mwili mmoja kunaondoa ubinafsi katika ndoa.

Furaha katika ndoa hutengenezwa. maana na msingi wa kuwaacha wazazi, kuambatana na mke na kuwa mwili mmoja katika ndoa vinapozingatiwa huleta furaha na kuepusha migogoro isiyo ya lazima katika ndoa. Ndoa ni ushirika na kuinuana ili kufikia malengo. Kufanikiwa katika ndoa juhudi ya wanandoa wote wawili inahitajika. Ni lazima wote wawili watamani na kutaka ndoa ikue na kuwa yenye furaha.

Kila mmoja katika ndoa ni lazima ajitahidi kwa bidii zake zote, hali akishirikiana vema na mwenzi wake katika kukabiliana na changamoto zote katika ndoa na kujitahidi kuufanya uhusiano wao kuwa mwema zaidi.

Wanandoa wafurahiane na kujifunza namna ya kutawala hisia zao na kumtanguliza Mungu ambaye ndiye muasisi wa taasisi hii ya ndoa. Kumbuka, hatuwezi kufanikiwa katika ndoa Mungu asipohusika.

***Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Chail Care Foundation (Tam-Care) inayojihusisha na masuala ya Ndoa na Malezi ya Watoto. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa barua pepe: info@tamcare.or.tz***

# MAISHA

NOVEMBA 22, 2020

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




## HARUSI

Ukurasa 12



**Namna ya kuandaa saladi ya Sausage**


Ukurasa 14



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Jinsi ya kusafisha choo na bafu katika nyumba



# Papai linatosha kukamilisha ndoto zako

Ukurasa 14

# Chunguza kwa nini mwanao anaokota hela?

**Na Moses Ismail**

MZAZI wake anasema; "huyu ana bahati ya kuokota hela, haipiti wiki lazima ataokota hata shilingi miatano." Ni kweli, 'ana bahati' ya kuokota hela. Vipi isiwe bahati wakati kila wiki anakuja na kumpa mama yake noti ya ama Sh. elfu moja, elfu mbili, elfu tano au elfu kumi alizosema "ameziokota pale"?

Katika wakati huu, wa ugumu wa maisha, mzazi, mama au baba anapokea pesa hizo kwa furaha na anapo zichenji anatoa angalau Sh. mia mbili hivi na kumpa akanunue 'chama' au kitu chochote anachotaka.

Kwa vile mara kadhaa fedha hizo zimesaidia 'kuikoa' familia kwa kununulia vitu muhimu ili kupata mlo wa siku, mama mtu amejenga mazoeya ya kumuuliza kila anaporudi; "leo hujaokota hela?" Anaamini mwanae ana bahati.

Lakini wakati mzazi huyu anapomsifia mtoto wake kwa bahati hiyo ya kuokota hela kwa wapangaji wenzake, hakuna hata mmoja katika yao anayeonyesha kuisikiliza 'hadithi' yake kwa msisimko, wananyamaza kimya kama hawakusikia kitu.

Wataonyesha vipi hisia za msisimko juu ya hadithi hiyo wakati katika 'vikao vyao vya kuteta' wameshamsema sana mtoto huyo kwa tabia zake za udokozi wa fedha anapoingia vyumbani mwao?

Mfano mama Kidawa juzi alipopoteza Sh. 1,500 zake alizorudishiwa na muuza mboga, pale kibarazani akichambua mboga zake, kwa nini alikimbilia kumuuliza mama wa mtoto huyo kama mwanae hajaokota hela yo yote?

Ndio, aliuliza hivyo kwa sababu wakati alipokuwa kibarazani alimuona mtoto huyo akicheza karibu yake na ghafla ndio hela zake zikayeyuka, akajua tu ni yeye aliye zikwapua.

Baada ya swali hilo, mama mtu alitoka na noti moja ya Sh. 1,000 na sarafu ya sh. 500 na kumpa mama Kidawa huku akisema: "Mwenzangu kumbe hela zako, mwanangu aliziokota, labda zilipeperuka, si unajua ana bahati ya kuokota hela!"

Na mama mtu anapotoa jibu hilo, analitoa kwa dhati kabisa ya kuamini kuwa mwanae ameokota fedha hizo na haijawai kumpitia kwenye fikra zake kama ana tabia ya udokozi. Hilo halijawahi kupita kabisa kwenye njia za ubongo wake.

Litampitiaje wakati hakuna hata siku mmoja mtoto huyo aliwahi kuiba hata Sh. 100 ndani kwao ingawa huwa wana tabia ya kuweka hela juu ya meza na hata juu ya kabati, chumbani, na wanazikuta pale pale?

Wakati mama huyu hafikirii hilo, majirani nao wanamshangaa kwa 'uzuzu' wake wa kuamini kuwa eti mwanawe ana bahati ya kuokota hela bila hata kujiuliza bahati hiyo inatokea vipi kwa mwanae tena kila wiki?

Ni kweli watoto huwa wanaokota hela, lakini ikitokea mwanao 'ana bahati' ya kuokota mara kwa mara, jaribu kujiuliza anaokota kweli? Mbane sana, jitahidi akueleze ukweli utakaokuingia akilini, maana watoto wadokozi huanza hivyo.

## NA HAMIS KIDAGO

0657 207168

## QUIZ

### Le quiz du week

1. Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel

Présent

Je ..................

Tu ..................

Il/elle ..................

Nous ..................

Vous ..................

Ils/ells ..................

Passé

J' ..............................

Tu ..............................

Il/elle ..............................

Nous ..............................

Vous ..............................

Ils/elles ..............................

2. Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
- Présent =
- Passé = ..................

3. Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.
- Présent = ................
- Passé = ..................

..................

4. Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
- Présent = .............

.............

.............

- Passé = ..................

..................

..................

### Majibu ya wiki iliyopita

Le quiz du week – end

- Nyumbua kitenzi "Être" kama maelekezo yanavyoonesha hapo chini.

Conditionnel

Présent

Je serais

Tu serais

Il/elle serait

Nous serions

Vous seriez

Ils/ells seraient

Passé

J' aurais été

Tu aurais été

Il/elle aurait été

Nous aurions été

Vous auriez été

Ils/elles auraient été

- Nyumbua kitenzi "Être" katika "Infinitif" présent na passé.
  - Présent = être
  - Passé = avoir été
  - Weka kitenzi "Être" katika Participe présent na passé.
  - Présent = étant
  - Passé = été

  ayant été

- Pangilia kitenzi "Être" katika Impératif présent na passé.
  - Présent = sois

  soyons

  soyez


  - Passé = aie été

  ayons été


  ayez été

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA KIDOGO



Zanzibar ipo upande gani katika bara la Afrika?

MKE mwenye wivu amejikuta akiumbuka mchana kweupee

**Mke:** Hivi mume wangu uko njr una wanawake wangapi?

**Mume:** Kama nywele za kichwa changu.

**Mke:** Akachukua nguo zake akaondoka kwa hasira, alipofika kituo cha basi alikumbuka mumewe alikuwa na kipara.

Alirudi kwa mumewe na kuomba msamaha.

# MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



## Tumewatoa wakwe kijijini sasa, wamegeuka wanataka mali zetu!

KARIBU tena msomaji tufurahie safu yetu ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo natupia jicho anga za wakwe wanaobebwa lakini asilani hawabebeki.
Baada ya kufurahia vinono, ghafla wanasahau kule wenyeji wao walikowatoa.
Kabla ya yote, hebu nitoe maelezo kidogo kukuelewesha ufanye nini pale unapoishi aidha na baba mkwe au mama mkwe au inapotokea unaishi na wote wawili.
Mara zote, huwa haishauriwi wakwe waishi na wanandoa hasa ndoa changa. Lakini katika tamaduni za Kiafrika, yapo mambo hutokea ambayo yanalazimu kuishi na wake ama kwa muda au milele.
Ziko sababu kadhaa zinazoweza kufanya wakwe waishi na wanandoa. Kwa mfano, pale mtoto wa kwanza anapozaliwa kwenye ndoa, msaada wao unahitajika jinsi ya kumhudumia mtoto.
Vilevile pale wazazi wa mwanamume au mwanamke wanapokuja kuishi na wanandoa ili kupata msaada wa matibabu kutokana na ugonjwa.
Pale wazazi wanapokuwa na hali mbaya ya umasikini huko vijijini na pale wazazi wanapokuwa wamezeeka na hawawezi kujihudumia.
Endapo wakwe zako wataendelea kukaa kwako kwa muda usioeleweka, yako mambo au hatua za kuchukua ili kuepuka migogoro ambayo inaweza kutokea na kusababisha matatizo kwenye familia yenu. Kwa ujumla unatakiwa umwombe sana Mungu akupe hekima ya jinsi ya kuishi na wakwe zako.
Mpenzi msomaji, baada ya utangulizi huo, sasa nikumegee kituko cha wakwe waliokaribishwa kutoka kijijini na kupatiwa hifadhi baada ya hali ngumu ya maisha, lakini sasa wanakuwa king'ang'anizi, tena wanataka kupora mali.
Baba mmoja, msomaji wetu mzuri wa gazeti hili alinitumia ujumbe mfupi wa simu ya kiganjani akielezea wakwe (wazazi wa mkewe) na hasa mama mkwe, alivyolazimisha kutwaa mali, japokuwa yeye na mumewe walishawawezesha kwa kuwajengea nyumba yao.
Ujumbe huo ulisomeka: "Kisa changu kinahusu wakwe zangu kuwatoa kijijini ili niwasaidie mimi na mke wangu, pamoja na kusomesha wadogo wanne wa mama watoto. Tumewahudumia hadi wamesoma tena shule nzuri wengine wameshaanza kazi. Ni miaka takribani saba. Ghafla wakwe hawa wanadai pale nilipowafikishia ni eneo lao na nyumba zote tatu nilizojenga mimi ni zao."
Baada ya ujumbe huu ilibidi nizungumze na wanandoa hawa kwa nyakati tofauti kupata kisa kizima. Wakasema wameishi na wazazi hawa upande wa mke kwa miaka saba sasa. Waliwatoa toka kijijini huko Singida baada ya maisha kuwa magumu na kuwaleta kuishi karibu nao.
Mmoja wa wanandoa hawa ambaye alijitambulisha kwa jina la Veronica, akasema shida kubwa iko kwa mama yake mzazi na mama mdogo ambao wanadai nyumba ambazo zilijengwa na wanandoa.
Veronica yeye anasema baada ya kuishi karibu na wazazi hao kwa muda, alitafuta eneo akawajengea wazazi wake nyumba huko Mkuranga.
Akawawekea huduma zote muhimu, umeme na maji.
Akawapeleka huko wazazi hawa lakini sasa wametoka huko wakidai ni porini wanataka kuishi karibu nao tena.
Wakati huo huo, yuko mama mdogo ambaye wakati fulani aliambiwa atafute eneo na wanandoa hawa ili zijengwe nyumba. Mama mdogo huyu alipopata eneo akarudi kuchukua fedha toka kwa wanandoa akanunua, lakini cha ajabu hati ya ununuzi akaandika majina yake na si ya mtoa fedha ambaye ni wanandoa (Veronica na mumewe) ila hati hiyo aliikabidhia kwa Veronica.
Likanunuliwa eneo lingine kwa mtindo huo huo na hati mama mdogo akaandika majina yake na kuikabidhi kwa Veronica. Katika maeneo yote hayo zilijengwa nyumba na wanandoa, hivyo hakuna hata senti moja ya mama mdogo.
Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha juu ya mzozo huo. Unasaidia kwa nia njema lakini unaambulia misukosuko. Maisha Ndivyo Yalivyo.
Wiki iliyopita nilisema kuwa hakuna tatizo lisilokuwa na chanzo.
Katika mzozo huu, naona kabisa roho ya umasikini imesimama mbele ya familia hii ya wakwe. Pamoja na mama mkwe kujengewa nyumba lakini bado alikataa akidai ni porini.
Roho ya umasikini ni mbaya sana. Huridhiki na kile unachopewa. Huinuka na kumshusha mtu pale anapokaribia mafanikio yake. Ni roho inayofanya uishi kwa kusaidiwa na watu, huwezi kujisimamia.
Niishie hapa msomaji wangu, ukiwa na ushauri, kisa nitumie kupitia 0715268581. Tukutane wiki ijayo.

# NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



## Viongozi wa dini waingilie kati ukatili kwa wanawake na watoto

MAADHIMISHO ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zinaanza Novemba 25 hadi Disemba 10, mwaka huu, ambazo zitafanyika kwa namna tofauti tofauti.
Kaulimbiu ya Maendeleo ya mwanamke ni faida kwa jamii nzima, kwa utambua kuwa mwanamke anashiriki shughuli za uzalishaji na mchango wake kwa maendeleo ya jamii yake.

Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ni kampeni ya kimataifa inayoongozwa na kituo cha kimataifa cha wanawake katika uongozi tangu mwaka 1991.

Chimbuko la 16 za kupinga unyanyasaji wa kijinsia na mauaji ya kinyama ya kinadada wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominica mwaka 1960.

Mwaka 1991 Umoja wa Mataifa (UN) ulichagua Novemba 25 iwe Siku ya Kimataifa ya kupinga ukatili wa kijinsia na kilele chake ni Desemba 10 ya kila mwaka.

Maadhimisho haya hutoa mwanga wa uelewa kwa jamii kwa siku nyingine muhimu kama Novemba 29 Siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Wanawake, Desemba Mosi Siku ya Ukimwi Duniani, Desemba 6 Siku ya Mauaji ya Kikatili ya Montreal 1989 (wanawake 14 waliuawa na mtu aliyekuwa anawachukia wanawake) na Desemba 10 Siku ya Haki za Binadamu Duniani.

Lengo la maadhimisho haya ni kutoa fursa kwa wanawake, wanaume, vijana wa kike na kiume na wanaharakati wengine kukuza uelewa wa umma juu ya mchango wa wanawake katika maendeleo na kutafakari matokeo ya harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi.

Jana, mabalozi wa nchi za Ulaya walikutana na kufanya mkutano na wanahabari jijini Dar es Salaam, kueleza mchango wa nchi zao katika kuinua wanawake, changamoto zilizopo na namna wanavyoshiriki kuzitatua.
Kila nchi ilieleza umuhimu wa mwanamke na namna gani ni muhimu kumwezesha au kumshirikisha kikamilifu katika kuyafikia maendeleo na kubwa zaidi ni kushirikishwa katika maendeleo ya jamii yake.
Ziko changamoto nyingi bado zipo katika nchi zinazoendelea kama Tanzania kwa kuwa bado ushiriki wa mwanamke katika ngazi za maamuzi siyo wa kiwango kinachotakiwa kufikiwa cha 50 kwa 50.
Jitihada nyingi zimefanyika lakini bado wanawake wameachwa nyuma katika ngazi za maamuzi, na si kwamba hawawezi au sifa za vyeti na uzoefu hawana bali ni kutoaminika au kujengwa mifumo ya kumfanya kuwa kiumbe dhaifu.
Mara zote palipo na maslahi mila hutangulia. Mathalani inapotoka jambo la kugawa mali za mirathi ndipo mila na utamaduni hukumbukwa maana yake ni kutaka kumpunja mmoja na kumpendelea mwingine kutegemeana na mazingira.
Siku hizi zinaadhimishwa wakati matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yanaongezeka, jambo ambalo linaonyesha kuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha wanawake wanaonekana kama watu na si vitu.
Yako baadhi ya makabila bado yanamwona mwanamke kama kitu na si binadamu ambaye ana mchango mkubwa na wa thamani kwa jamii na taifa kwa ujumla.
Mathalani, hivi karibuni mkoani Arusha mume alimshambulia mkewe na kumkata mkono kwa kile kilichodaiwa ni wivu wa mapenzi.
Lakini tukio lisilosahaulika kirahisi ni la Kigamboni, Jijini Dar es Salaam, kwa mwanamume kumuua mkewe na kumchoma kwa gunia la mkaa, ambaye aliungua na kuteketea kabisa.
Haya ni baadhi ya matukio kati ya mengi ambayo ni tishio kubwa kwa jamii, na yanaonyesha bado kunakazi kubwa ya kufanya ambayo lazima viongozi wa dini washiriki.
Viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kugusa moyo wa muumini na kumbadili kutoka matendo flani mabaya hadi mazuri, na kwa nafasi hiyo ni lazima sasa kuisaidia jamii katika mafundisho ya dini juu ya hiki kinachoikumba jamii kwa sasa kwamba kuua ni jambo la kawaida sana.
Maadhimisho haya yanafanyika huku kukiwa na wakati mgumu katika malezi ya watoto wa kike na kiume, kwa sasa wanalawitiwa na kubakwa, wengine ni watu wa karibu kabisa ambao hutumia ukaribu na watoto kuwaharibu.
Wiki iliyopita mkoani Lindi, kijana wa miaka 23 alikamatwa kwa madai ya kumlawiti mtoto wa miaka sita. Tukio kama hili linafikirisha sana kwamba unawezaje kutenda unyama kiasi hiki?
Lingine ni la mkoani Morogoro mwanafunzi kulawitiwa na mtu ambaye alikuwa akimfanyia hivyo kila mara, huku ikielezwa kuwa matukio hayo ni mengi mkoani humo kwa wanafunzi wa shule za msingi.
Gazeti hili liliwahi kuandika ripoti maalum ya matukio ya kulawiti watoto wilayani Kisarawe, jambo ambalo linaonyesha bado kuna kazi kubwa ya kufanya.
Ni muhimu na lazima siku 16 za kupinga ukatili zitumike vizuri kuifikia jamii, kutoa visa mkasa na shuhuda ambazo zitasaidia kubadili fikra ya jamii ambayo ndiyo mlezi wa watoto.









Mfanyakazi wa gazeti la The Guardian, Henry Mwangonde, alipofunga pingu za maisha na Josephine James, Novemba 14, katika Kanisa la Moravian, Iyela Mbeya.

# MITINDO



## MWANAMUME NENDA HIVI KUJITAMBULISHA

JE, unafikiria siku moja kwenda nyumbani kwa mpenzi wako kujitambulisha? Kama ndiyo, vazi gani umepanga kuvaa ili utoke nadhifu?

Watu wengi wanapofikia katika hatua kama hii wanakata tamaa, na wengine wanatumia gharama kubwa kutafuta mavazi. Lakini kuna hatua rahisi ambazo ukizifuata unatumia gharama ndogo, huku ukijihakikishia siku hiyo unakuwa na furaha ya mafanikio.

Hizi ni baadhi ya mbinu unaweza kuzitumia wakati unachagua mavazi ambayo utayatumia kwenda kujitambulisha kwa mpenzi wako.

1: Kama unataka kutoka kiheshima zaidi, vaa suti iliyopangiliwa vyema kwa rangi. Rangi nzuri ni nyeusi, udhurungi, nyeupe na bluu bahari.

Usivae suti yenye rangi ya kung'aa sana kwani itakuondolea hali ya kujiamini na kujiona uko tofauti na wenzako.

2: Kama unataka kuvaa nguo za kawaida, suruali ya kitambaa na shati la pamba ni chaguo zuri kwako. Rangi inayopendeza ni Nyeusi, Bluu mchanganyiko, maziwa au samawati.

3: Kama ni mpenzi wa nguo za asili unaweza kuvaa za vitenge au khanga iliyoshonwa vizuri. Chagua rangi zisizong'aa sana ili kukupa furaha zaidi.

Tukio hilo likiwa la kifamilia zaidi, unaweza kuvaa nguo ya ubunifu na yenye mvuto zaidi kwa sababu itakupa nguvu na mvuto wa kipekee.

## UREMBO

# NGOZI NYORORO

# Papai linatosha kukamilisha ndoto zako

PAPAI ni moja ya tunda tamu linalopatikana katika ukanda wa Tropiki. Tunda hili linaliwa kwa wingi kama kiburudisho baada ya chakula.

Watu wengi wanafahamu matumizi ya papai ni kwa ajili ya kuliwa ili kumuongezea mlaji vitamin C na E, lakini kuna matumizi mengine ambayo humpatia mtu faida kubwa.

Moja ya matumizi sahihi ya tunda la papai ni kuboresha ngozi na kumfanya mtu kwa na muonekano mzuri na wenye uasilia kwa kugeuza kuwa kilainishi.

Unaweza kutumia bidhaa zitokanazo na Papai kama sabuni, mafuta ya mwili, tona, 'moisturizer' au 'facial peels' kwa ajil ya kujisugua.

Ukitumia maski ya papai utakuwezesha kutunza sura na kuwa na muonekano mzuri, pia inasaidia kurudisha ngozi ambayo imeanza kupata makunyanzi.

JINSI YA KUTUMIA

Ni rahisi kutengeneza maski ya papai na ukitumia itakusaidia katika kukabiliana na ngozi iliyoanza kuchoka na kung'arisha ngozi .

Maski ya mchanganyiko wa papai na yai ni nzuri katika kuhakikisha unakuwa na ngozi nzuri na nyororo zaidi.

Chukua papai ulikate kisha toa mbegu; yaani kokwa zake na ulisage kwa kutumia blenda au pondaponda kwenye bakuli kwa kutumia mchi.

Kisha weka mchanganyiko huo kwenye bakuli. Vunja yai na ukoroge kuhakikisha kuwa mchanganyiko huo umechanganyika vizuri.

Safisha uso wako, kisha paka maski usoni na unapopaka hakikisha mchanganyiko huo haugusi macho

Kaa kwa dakika 15 kabla ya kuosha na kujifuta kwa kutumia taulo safi.

Baadaye paka mafuta ya papai au yale ya kawaida.



## MAPISHI

## Na Mary Geofrey

# NAMNA YA KUANDAA SALADI YA SAUSAGE

SALADI ni chakula chepesi, kinakupa nguvu za kutosha na kuzuia adha zinazotokana na kushiba kupita kiasi.

Chakula hiki kina nyama kiasi ambayo inaweza kukupa nguvu zaidi, hasa kwa wale wanaopenda kula nyama katika kila mlo.

**Mahitaji**

Kabichi, nyanya, vitunguu, spinach, pilipili hoho, Mafuta ya Oliva, Limao au vinegar au ndimu, chumvi kiasi na Soseji

**Namna ya kuandaa**

Anza kuandaa soseji kwa kuzichemsha na maji, weka chumvi kiasi na acha ziive.

Kata mboga za majani kwenye vipande vidogo na weka kwenye sahani.

Kata nyanya, pilipili hoho, karoti kwenye vipande vidogo, kisha changanya na salad yako.

Kata soseji kwenye vipande vidogo na changanya kwenye salad

Changanya vinegar, limao au ndimu na mafuta ya Olive pembeni kwenye bakuli kisha koroga vizuri hadi ziwe sawia.

Nyunyuzia mchanganyiko wa limao au ndimu au vinegar na oil juu ya salad. Nyunyuzia kuzunguka salad, usirundike sehemu moja.

Weka chumvi kiasi kisha anza kuchanganya


Kumbuka, salad inaliwa ikiwa ya baridi, hauna haja ya kupasha moto.



# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

## JINSI YA KUSAFISHA CHOO NA BAFU KATIKA NYUMBA



USAFI wa nyumba wa mara kwa mara ni nguzo kubwa ya kuistawisha na kuipendezesha. Isipofanyiwa usafi wa mara kwa mara, huchakaa mapema na hata kuharibika kabisa.

Lakini leo nitapenda kuzungumzia baadhi ya dondoo za namna ya kusafisha katika sehemu ya bafu na choo.

Kabla ya kuanza kusafisha bafuni, kwanza ondoa vitu vyote vya kuhamishika kama vile vizulia, tenga la nguo chafu, meza au kabati na ndoo ya taka, huku wakati huo ukihakikisha dirisha liko wazi ili hewa ipite kuondoa hewa nzito.

Baada ya hapo unaweza kuondoa buibui kwenye kona za dari ikifuatiwa na kufuta vumbi mlango katika sehemu ya ndani na nje.

Wakati wa kusafisha ni vyema kuanzia juu na kushuka chini ili kuruhusu taka za vumbi na buibui zimwagike sakafuni kwa ajili ya kusafisha mwishoni. Katika kufanya hivyo, unapaswa kutumia kitambaa kufutia au fagio.

Unaweza kumiminia sabuni za kusafishia kwenye bakuli la choo na kuiacha kwa dakika kadhaa ili uchafu ulainike.

Weka dawa ya unga wa kusafishia katika sehemu zenye uchafu ili iwe rahisi wakati unasugua.

Ni vyema ukazingatia maelezo ya dawa ya kusafishia ili kuwa na uhakika unatumia kiasi sahihi ambacho hakiwezi kuharibu.

Katika kuta za bafu pia unapaswa kupaka sabuni au dawa nyingine za kusafishia endapo zitakuwa za marumaru na kwa kutumia sponji au brashi unaweza kusugua sehemu uliyoweka sabuni hiyo huku ukihakikisha unaisuuza kuondoa michirizi yote michafu. Kama ukuta ni wa karibu na sinki au bakuli la choo, ukaushe kwa taulo.

Ni muhimu kukumbuka kuvaa glovu wakati wa kusugua kwani baadhi ya dawa na sabuni zinaweza kuchubua ngozi.

Pia, mswaki wa zamani usiotumika unaweza kutumika kuondoa uchafu kutoka eneo la kati ya bomba na mishikio yake na unapaswa kuepuka kutumia brashi ya kusugulia bakuli la choo, kusugulia sinki kwa sababu unaweza kusambaza maradhi.

Safisha kioo kwa kutumia ama maji na taulo au dawa ya kusafishia vioo na taulo.

Safisha nje ya choo ukianza na ile sehemu ya juu ya kuvuta maji. Kwa taratibu unaweza kuendelea kusafisha eneo lote la nje ya choo ambalo ni pamoja na mfuniko na eneo la chini ya sehemu ya kukalia na kupafuta na taulo.

Kwa upande wa sakafu, hakikisha usafi wako unaanzia sehemu zilizojificha hadi zile za wazi na ni vyema kusafisha vumbi na uchafu wote ulio chini ya eneo la choo kilipoungana na sakafu.

# MPANGILIO

## DONDOO MUHIMU YA KUPAMBA NDANI YA SEBULE YAKO.

1: Weka mambo ya kisanaa kama michoro, sanamu za kuchonga na vitu vya kiasili ili kunogesha varanda yako.


2: Weka makabati ya kuwekea vitabu, magazeti na vitu ambavyo vitawafanya watu kupanua akili zao kwa kujisomea.

3: Weka maua ya sili kwa kupanda kwenye mitungi ya ndani, pia unaweza kuweka miti midogomidogo ili kupendezesha zaidi.

4: Unaweza kuweka vyombo vidogogo kama ala za muziki, sahani za mapambo na vitu vingine vyenye nakshi ya kupendeza.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
DOKTA ULINIULIZA TATIZO LA PRESHA, SUKARI, SHINIKIZO NA UNYONG'ONYO LIMENIANZIA WAPI, "NDIO HAPA"
KWANI UNGESEMA 'UMEGALAGAZWA' NISINGEKUELEWA MPAKA UNILETE MPAKA HAPA!
DALADALA ZINAVYO-PITA BILA KUSIMAMA NI DHARAU AU?...
AU WANAONA SANAMU LIME-KAA KITUONI?
HII NYUMBA ULIYONIJENGEA UKAWEKA PAKING' NI UREMBO?
YA'MKE WANGU HATA SEBULE HAINA!
DANGA
KWELI WEWE MWANASIASA
MIMI NDIO MZEE WA AHADI TAMU TAMU MUDA WOTE "ZEE LA MMA"
MAWAZO YA NINI, 'KIKOKOTOO' KIKIISHA UTARUDI KWA MKEO AKAKUBEMBELEZE
NNAVYOMJUA ATAUA!
JAMANI MLIONIPIGA CHINI NAPITA KUWASABAHI WAJUMBE MPO?
UNATAKA MPANGAJI MWENYE MKE UMEMUOLEA?
'ATII?'
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...TETA KWA SAUTI UZOE SIFA...

HABARI KIMATAIFA

## Erdogan, Mfalme Salman wazungumza

**ANKARA,** Uturuki

RAIS wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, amezungumza kwa njia ya simu na Mfalme Salman wa Saudi Arabia (pichani chini), kabla ya kufanyika mkutano wa kilele wa kundi la mataifa yanayoinuka kiuchumi duniani yanayofahamika kama G20.

Saudia itakuwa mwenyeji wa mkutano huo unaofanyika kwa njia ya video.

Kwa mujibu wa ofisi ya Erdogan, viongozi hao wawili wamejadili namna ya kuboresha uhusiano baina ya mataifa yao mawili.

Uhusiano kati ya Uturuki na Saudi Arabia ulizorota kwa kiwango kikubwa baada ya kuuawa kwa mwandishi wa habari wa Saudi Arabia, Jamal Khashoggi, katika ofisi za ubalozi mdogo wa Saudia mjini Istanbul mwaka 2018.

Pia Uturukia inalaumiwa kwa kuwaunga mkono kundi la Udugu wa Kiislamu, ambalo serikali ya Saud Arabia inaliona kama kundi la kigaidi.

Lakini taarifa hiyo ilisema viongozi hao wamekubaliana kufungua milango ya majadiliano na kuboresha uhusiano wao. **DW**



## India yailaumu Pakistani kwa uchokozi

**MOMBAI,** India

INDIA imeituhumu jirani yake kwa kuhusika kwa kifo cha mwanajeshi wake mmoja na mwengine kujeruhiwa kufuatia shambulizi lililotokea upande wa Pakistan.

Mauaji hayo yametokea katika eneo lenye operesheni nyingi za kijeshi lenye kuligawa jimbo la Kashmir ambalo mataifa hayo mawili yenye nguvu za nyuklia wanadai kila mmoja ni mali yake.

Msemaji wa jeshi la India, Luteni Kanali Devender Anand, alisema wanajeshi wa Pakistan, walifyatua makombora ya mizinga na silaha nyingine katika maeneo ambayo nchi yake inadhibiti kusini mwa Wilaya ya Rajouri.

Anand alikiita kitendo hicho kuwa cha uchokozi na ukiukwaji wa makubaliano ya kusitisha mapigano ya mwaka 2003.

Alisema jeshi la India walilipiza kisasi kwa tukio hilo.

Hata hivyo Pakistan hadi sasa haijasema lolote kufuatia mkasa huo. **DW**

# Polisi wa Uganda wana haki kuua

**KAMPALA, Uganda**

WAZIRI wa Usalama wa Uganda, Elly Tumwine, amesema jeshi la polisi linaweza kuchukua hatua kali ikiwamo kuua endapo ghasia zitafika kiwango fulani cha hatari.

Kauli ya waziri huyo, imekuja siku tatu baada ya polisi kukabiliana na waandamanaji na kuwaua watu 37 hadi kufikia jana.

Virugu hizo ziliibuka baada ya kukamatwa kwa mgombea urais wa upinzani Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine siku ya Jumatano wiki hii.

Kyagulanyi, alishtakiwa kwa kukiuka kanuni za afya za kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona katika mkutano wa kampeni.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu yanasema hatua ya kukamatwa na kushitakiwa kwa Bobi wine ni kisingizio cha kukandamiza upinzani kabla ya uchaguzi mkuu wa mwezi Januari.

Kyagulanyi, ni miongoni mwa wagombea 11 wanaopambana kumuondoa madarakani Rais Yoweri Museveni, ambaye aliingia madarakani mwaka 1986.

Hata hivyo, Bobi Wine aliachiwa kwa dhamana juzi baada ya kufikishwa mahakamani.

Kukamatwa kwake kulisababisha maandamano ya vurugu yaliyofanywa na wafuasi wake.

Vikundi vya vijana walifunga barabara na kuchoma moto matairi ya magari katikati ya mji wa Kampala, na maeneo mengine nchini humo.

Vikosi vya usalama vilijibu kwa kurusha mabomu ya machozi na kutumia risasi za moto kuwatawanya watu. Katika ghasia hizo polisi 11 walijeruhiwa.

"Polisi wana haki ya kukupiga risasi na kukuua ukifikia kiwango fulani cha ghasia, wataka nirudie? Polisi wana haki ya kukupiga risasi na kukuua na utakufa bure usiseme hukuambiwa," alisema Waziri huyo.

Taarifa ya polisi ilisema ni watu 28 waliofariki katika maandamano hayo, lakini shirika la habari AP limemnukuu mfanyakazi wa chumba cha kuhifadhia maiti akisema walihesabu miili 37 ya watu waliokufa. **BBC**



Wanajeshi wa Ethiopia wakiwa kwenye kifaru wakati wakielekea mji mkuu wa jimbo la Tigray jana. **PICHA: DW**

# Wanajeshi wadhibiti mji wa pili

**ADIS ABABA,** Ethiopia

SERIKALI ya Ethiopia imetangaza kuudhibiti mji wa pili kwa ukubwa katika jimbo la Tigray ambao umekuwa ukigombaniwa tangu mwanzoni mwa mwezi Novemba.

Taarifa kutoka ofisi ya Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Abiy Ahmed, ilisema kupitia televisheni ya taifa kuwa vikosi vya usalama vimechukua udhibiti wa mji wa Adigrat na vilikuwa vinaelekea katika HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/vikosi-vya-ethiopia-vyaelekea-mji-mkuu-wa-tigray/a-55647864" mji mkuu wa jimbo la Tigray wa Mekele.

Hatua ya serikali ya Ethiopia kuendelea kushambulia jimbo hilo, inaonyesha hakuna dalili zozote za kukubali shinikizo la kimataifa la kusitisha mapigano katika mgogoro huo.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu huyo, alilipongeza jeshi la serikali ya shirikisho kwa kusonga mbele, akisema sasa vikosi vyake vimeikomboa Adigrat kutoka kwenye mikono ya chama cha Ukombozi wa Watu wa tigray (TPLF).

Abiy alisema kwa kushirikiana na Waithiopia wote watahakikisha mahitaji yote ya kibinadamu yanashughulikiwa.

"Usalama na ustawi wa jumla wa watu wa Tigray ni muhimu sana kwa serikali ya shirikisho na tunafanya kila linalowezekana kuhakikisha utulivu unapatikana kwenye Mkoa wa Tigray na kwamba raia wetu hawapati madhara yoyote," alisisitiza Abiy.

Wakati huo huo, Umoja wa Afrika (AU) umetangaza kuwa utapeleka wajumbe maalum kupatanisha pande mbili hasimu ili ipatikane suluhu ya kudumu.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Umoja huo ulisema jukumu la msingi la wajumbe hao litakuwa kuzishirikisha pande zote zinazohusika katika mzozo huo na kuandaa mazingira ya kufanyika mazungumzo ya kitaifa ya kutatua masuala yote yaliyosababisha kuibuka kwa mapigano hayo. **DW**

# Ruvuma Mpaka Maputo na kumbi zilizotikisa Dar



Na Adam Fungamwango

TUNAANZA kumtazama mwanamuziki nguli nchini, Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kiki', ambaye kwa sasa ni mgonjwa, akiwa amejipumzisha nyumbani kwake maeneo ya Mtoni jijini Dar es Salaam.

Kwanza kabisa tumpe pole na kumuombea kwa Mungu amponye na maradhi yanayomkabili.

Moja ya vibao vyake vikali alivyovitoa mwanzoni mwa miaka ya 1980, ni ule unaoitwa 'Mtoto wa Mjini.' Wimbo huu unaeleza kila kitu. Unaeleza wakati huo Dar es Salaam ilivyokuwa ikichemka kama bahari. Ni kwamba pamoja na wakazi wengi wa Dar es Salaam kuwa na kazi maalum za kufanya kutokana na kuwa na mashirika mengi binafsi na ya umma, lakini pia walipenda mno starehe ya muziki wa dansi.

Kiki anasema bendi zimetapakaa kila kona ya Dar. Kumbi za starehe ziko za kutosha maeneo yote. Pia watu wanajaa kwenye kumbi zote hizo, kana kwamba wanaingia bure.

Msanii wa hip hop, Profesa Jay, yeye mwanzoni mwa miaka ya 2000, alikuja na ngoma yake aliyoiita 'Bongo Dar es Salaam', moja ya mistari yake ni ile inayosema 'Sinza ya leo kila nyumba baa, na zote zinajaa, na hapo ndipo utakaposhangaa.'

Hivi ndivyo kumbi za burudani zilivyokuwa zikijaa kila wiki. Leo tutaziangalia kumbi za jijini Dar es Salaam tu. Iko siku tutazungumzia za mikoani pia.

Hapa unaweza kushangaa kitu kimoja tu. Zamani Dar haikuwa na watu wengi kama ilivyo sasa. Inakadiriwa kuwa miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1990 kulikuwa na wakazi 500,000 mpaka milioni moja. Pamoja na uchache huo, zaidi ya kumbi 100 jijini Dar es Salaam zilikuwa zinajaa. Watu walikuwa wanajua kutumia. Watu walijua kujirusha. Walijua kula bata. Wanafanya kazi wiki nzima, Ijumaa, Jumamosi na Jumapili zilikuwa siku ambazo wengi walikwenda kuburudika dansini.

Kwa sasa Dar inakadiriwa kuwa na watu milioni tano na baa zimekuwa nyingi mno kuliko hata mwanzo. Lakini kwa bahati mbaya sana bendi si nyingi tena kama zamani kwani kulikuwa na zaidi ya bendi 50 za watu binafsi, mashirika ya umma, kampuni, jumuiya za Chama Cha Mapinduzi na majeshi yote ya ulinzi na usalama.

Kutokana na bendi nyingi kupiga kwenye kumbi mbalimbali wakati huo na kutangazwa na gazeti moja tu wakati huo la Uhuru na Jumapili gazeti la Mzalendo, ingawa baadaye likaja pia gazeti la Mfanyakazi.

Bendi na magazeti haya kwa kiasi kikubwa yalisababisha kumbi nyingi jijini Dar es Salaam kuwa maarufu sana. Na hii ni kutokana na watu kutaka kujua bendi gani itapiga wapi na lini. Ilikuwa haiwezekani kutambua hilo bila kupata magazeti hayo.

Haikuzifanya kumbi au baa hizo kuwa maarufu wakati huo, lakini majina hayajafutika kwenye vichwa na mashabiki wengi wa muziki wakati huo ambao kwa sasa baadhi wako Dar na wengine wapo mikoani wakiendelea na harakati zingine za maisha.

Baadhi ya kumbi zilizotikisa wakati huo kwa bendi mbalimbali kwenda kupiga muziki wa dansi ni Ruvuma Mpaka Maputo Bar, iliyokuwa maeneo ya Vingunguti kuelekea Kipawa, wenyewe waliipachika jina la 'Njia Panda kwenda Airport.'

Kumbi zingine zilizovuma na kutemesha Dar na hazitoweza kufutika kirahisi kwenye akili ya mashabiki wa muziki wa miaka hiyo ni Maghorofani (Tandika), Makonde Bar (Msasani), Mbwisi Bar (Manzese), Mkirikiti Bar (Msasani), Muleba Bar (Mabibo), Mundo Bar (Temeke), Amana Social Hall (Ilala), Miembeni Bar (Ilala) na Ndendeule Bar (Mtoni).

Zingine ni Omax Bar (Keko), Sabasaba Bar (Mbagala), Safari Resort (Kimara), Sensera Bar (Tandika), Silent Inn (Mwenge), Super Stereo Bar (Temeke), Super Fanaka Bar (Buguruni), Super Mini (Temeke), Tumaini Social (Kiwalani), Uhemeri Bar (Luhanga), Wami Bar (Mwananyamala), White House (Ubungo), First Inn (Mburahati) na Kigogo Randa Bar.

Zingine ni CCM Kata ya 14 (Temeke), Highway Bar (Kurasini), Bondeni Bar (Kariakoo), DDC Keko, DDC Kariakoo, DDC Magomani Kondoa, DDC Mlimani, Dimax Bar (Tandika), Friends Corner (Manzese), Hotel 92 (Shekilango), Hunters Bar (Ubungo), Ikweta Bar (Mtoni), Kigongo Bar (Buruguni) na Makonde Bar (Mikocheni),

Historia ya ukumbi wa Wami Bar ni kwamba bendi nyingi zilikuwa zinapiga, lakini bendi pendwa zilikuwa mbili tu, kwanza kabisa Juwata Jazz Band ambayo ilikuwa ikipiga hapo mashabiki hufurika ndani hadi nje, lakini pia Super Matimila chini ya hayati Dk. Remmy Ongalla.

DDC Mlimani Park waka Sikinde waliwahi kupiga mara chache lakini kilichowapata, waliamua tangu siku hiyo kusikitisha kupiga ukumbi wa Wami Bar. Ipo siku nitasimulia kisa hiki.

Kumbi zingine ni, Mpakani Bar baadaye ikaitwa Silent Inn (Mwenge), Stereo Bar (Kinondoni), White House (Ubungo) uliokuwa ukitumiwa na Maquiz du Zaire, Shirikisho Bar (Vingunguti) Kwa Mama Bar (Vingunguti), Chabruma Inn, Chimoka Bar (Magomeni) kwa sasa inaitwa 'Travertine', Lang'ata Bar (Kinondoni), Jemelasi Bar 'Mtoni kwa Aziz Ally'. Pandia Bar (Buguruni) na Top Life Bar (Kinondoni Mkwajuni), Kimboka By Night na Sewa Bar (Buguruni).

Hizi ni kwa uchache tu kati ya kumbi nyingi za Dar es Salaam zilizokuwa zikipokea bendi mbalimbali.

Unaweza kukuta kila kumbi ina bendi kwa siku moja. Bendi Dar es Salaam kama nilivyosema zilikuwa nyingi mno, zingine zilikuwa zikitoka hata mikoani kwenda Dar kwani tayari zilikuwa zina mashabiki wengi kwa sababu ya nyimbo zao ambazo walizirekodi na kutamba sana redioni.

Bendi ziligawana mashabiki. Kuna zilizojaza sana. na zingine zilizopata mashabiki wa wastani. Lakini bendi karibu zote zinapata mashabiki. Hii ndiyo Dar iliyoliyokuwa ikichemka kama bahari kama alivyoimba King Kiki.

# Beba elimu yako uzeeke bila mali

Na Magabilo Masambu

MWANASAYANSI mashuhuri, Albert Einstein, alipoulizwa akili ni nini alisema: "Akili ni kile kinachobakia baada ya kuondoa yote uliyofundishwa darasani."

Kwa mujibu wa Einstein, unaweza ukawa na elimu lakini huna akili na vilevile unaweza ukawa na akili lakini ukakosa elimu.

Ukweli ni kwamba ni bora ukawa na akili ukakosa elimu kwa sababu akili ndiyo ilibuni elimu. Yaani watu wenye akili walikaa wakaweka utaratibu wa mtu kukaa darasani na kujifunza kwa kipindi fulani, kisha apimwe kwa mitihani na atunukiwe cheti. Ubunifu huo ulifanywa na wenye akili.

Ni ukweli kwamba dunia ina tatizo la ajira, kwa sababu ongezeko la watu haliendani na miundombinu yenye kutoa ajira, fursa za ajira ni ndogo kuliko mahitaji ya watu duniani. Ukweli kuwa hatuwezi kuwajiriwa wote uko wazi, hivyo ni lazima tuwe na watu wenye akili si wenye elimu watakaobuni shughuli ambazo zitaajiri wenye elimu na wasio na elimu.

Mwasisi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, katika kitabu chake cha 'Elimu ya Kujitegemea' ameeleza kwamba watu wengi wanatafuta elimu si kwa ajili ya kutafuta maarifa yawasaidie kutatua matatizo yao ya kila siku bali wanaosoma sana ili kujaribu kuyakwepa matatizo yenyewe. Yaani mwenye Diploma anasoma Digirii akiamini kwamba kwa kuipata digirii atakuwa amepunguza shida kwa kutegemea kipato kikubwa. Vivyo hivyo kwenye ngazi nyinginezo za juu kabisa kuufikia uprofesa!

Lengo la elimu si kuipata ili kukwepa matatizo bali kuitumia kutatua matatizo. Kama utakuwa na elimu ikashindwa kutatua changamoto zinazokukabili au zinazoikabili jamii, basi unaweza kuwa na elimu ukawa umekosa akili.

Tatizo kubwa tulilo nalo ni kubeba elimu zetu na mwisho tunazeeka bila mali. Hii ni kwa sababu wengi wenye elimu hudhani kwamba elimu zao ni kinga katika kujishughulisha na baadhi ya shughuli ambazo hufanywa na wenye akili wasio na elimu! Kumbe ni bora ukakosa elimu ukawa na akili unaweza kupata mali.

Uzoefu unaonyesha kwamba wenye elimu wengi wameajiriwa na wenye akili wasio na elimu lakini wenye elimu wamebaki kujisifu kuwa na vyeti vizuri bila mali. Tutaanza kuendelea tu pale tutakapokubali kwamba elimu zetu si kitu bali tunapaswa kutumia akili ili tupate mafanikio ya kimaisha.

Joseph Mayagira katika kitabu chake cha 'Kubuni Biashara Ikupasayo,' ameeleza thamani tano za kufanikiwa kibiashara. Jambo moja alioleeza mwandishi huyu anasema "Ili kufanikiwa kiuchumi ni kubuni kitu cha thamani kwa maisha ya watu." Hapa inahitajika akili kufahamu kwamba jamii ina changamoto gani ili kubuni biashara itakayotatua changamoto hiyo.

Kila anayesoma anatarajia mafanikio yatokanayo na elimu yake, lakini lazima tufahamu kwamba ukiwa na elimu pekee bila akili hautofanikiwa. Lazima uwe na akili ya kubuni namna ya kutatua changamoto zinazokuzunguka bila kujali una elimu kubwa kiasi gani.

Baadhi ya wanaojiita wasomi, wamesikika mara kadhaa wakisema hawawezi kufanya hiki na kile kwa kuwa wana elimu kubwa. Wengine wamekuwa wakikataa kuajiriwa kwa kuwa wanaona watalipwa ujira mdogo, huku wakiamini wana elimu kubwa bila kujua kwamba mwanzo wa kuwa na kikubwa ni kuanza na kidogo, ili kujitengenezea mazingira ya kupata kikubwa na hivyo hubaki bila ajira.

Tofauti kati ya wenye akili na wenye elimu ni kwamba wenye elimu kila wanalofanya lazima wahusishe na elimu yao. Lakini lazima tufahamu kwamba mfumo wetu wa elimu kwa kiasi kikubwa hauendani na mazingira tuliyo nayo.

Mfano unakuta tunajifunza wakoloni walivyotumia njia mbalimbali kututawala na tunafika vyuo vikuu kwa kufahamu vyema kueleza vizuri njia hizo, lakini uhalisia wa maisha katika kufanikiwa inamaana gani hasa? Kama tunataka kufanikiwa kwa kutumia elimu zetu lazima tukubali kwanza kubadili aina ya elimu tuliyonayo kisha tuitumie katika mazingira yetu.

Limekuwa jambo la kawaida kwa kijana aliyekulia kijijini akifanya shughuli za kilimo baadaye akaenda chuo kikuu na baada ya masomo kijana huyo anaona si halali tena kwake kufanya kilimo na kwamba si hadhi yake kwa sababu ni msomi! Si hivyo tu, anapewa heshima kiasi kwamba hata wazazi wanaogopa kumtuma.

Tubadili mtazamo tutabadili maisha, elimu iwe nyenzo ya kutuongezea ufahamu tu lakini isiwe tegemeo la kutupatia ajira kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeisaidia serikali kutatua tatizo la ajira kwa kujihusisha kwenye shughuli zenye kutatua matatizo mbalimbali kwenye jamii.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili. Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo.
Kutokana na mwenyewe kutokuwa na msimamo, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja - 9

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

"We Cecy unamjua vipi?"

"Sikiliza bwana wewe. Cecy ni mpenzi wangu mwaka mmoja sasa. Inaonekana wewe ndiye umevamia. Sasa nashangaa unanijia juu. Wewe ndiwe unatakiwa kuacha kutembea na mpenzi wangu."

Zahir alibaki kimya kidogo. Maneno hayo yalimwingia. Ni kweli mapenzi yake na Cecy yamedumu kwa miezi mitatu tu. Kwa sasa wana mzozo.

Kama kweli mapenzi ya kijana huyo na Cecy yana mwaka, basi yeye ndiye anatakiwa apewe ovyo la kutembea na mwanamke wa mtu na si kijana huyo anayempiga mkwara.

Hata hivyo, hakukubali. Wivu ulimshika. Pamoja na kwamba ni mpenda wanawake wengi, lakini alitokea kumpenda Cecy. Ni kwa sababu tu hawezi kurekebisha tabia aliyo nayo. Hata kama ni kicheche alitaka amdhibiti au kumtia mikononi mwake. Hakutaka mtu yeyote awe naye msichana yule mrembo. Akakata simu.

"Nitamuonyesha." Alisema kwa sauti kubwa kana kwamba kulikuwa na watu wengine chumbani kwake wakati alikuwa peke yake.

Alichofanya alipompora simu Cecy ni kitu kidogo tu. Kutafuta namba ambayo inapigwa au kupiga zaidi kuliko zingine. Aliipata ya Mashaka. Wala hakutaka kufikiri.

Alijua yoyote atakayekuwa anapigiwa au kupiga zaidi kuliko yeye, atakuwa ndiyo mpenzi wa msichana huyo. Hivyo ndivyo alivyoipata namba ya Mashaka.

Alichogundua Mashaka ni kwamba wakati Cecy alipokuwa akimdharau na kumzodoa, alikuwa ameangukia kwenye mikono ya fedhuli yule aliyempigia simu na kumwonya.

Akapimpigia simu Cecy na kumuambia kilichotokea.

"Achana na yule mwehu, asikusumbue." Yalikuwa maneno ya kukera kwa aliyeambiwa lakini ya faraja kwa Mashaka. Ni maneno ambayo yalimhakikishia uhakika wa penzi la Cecy kwake.

Penzi ni kitu kisicho na dhamana duniani. Huchanua na kunyauka. Hugeuka wakati wowote. Leo kwa huyu kesho kwa huyu. "Atajijua mwenyewe, sisi yetu yanatuendea." Ni maneno yaliyotoka kwenye kinywa cha Mashaka na kumfanya Cecy kuangua kicheko.

"Mashaka nawe. Hayo maneno huwa unayapata wapi?"

"Nayapata kwako." Alijibu na kusababisha wote wakauke kwa kucheka. Wakakata simu.

**************************

Mlio wa risasi ulisikika. Ni mshindo uliowastua wengi maeneo ya Magomeni Mikumi kituoni. Watu walikimbizana huku na huko, kila mmoja kuokoa maisha yake. Haikujulikana nani alipiga risasi hiyo. Nani alipigwa na kwa nini.

Wakati huo hakuna aliyekuwa na haja ya kuhoji. Kila mmoja alikimbia bila kujua anakimbilia wapi. Lengo ni moja tu. Kuokoa uhai. Kila mmoja alikokombilia alidhani kuwa ndiko kwenye usalama. Cha ajabu ni kwamba wengine walikimbilia ambako wengine nao wanatoka. Na wao wanakimbia pia. Walipishana kati. Hakuna aliyejua hatari hasa inatokea wapi.




**"Mashaka wangu weee, Mashaka unaondoka unaniacha na nani? Mashaka amka basi kidogo nikubusu. Mashaka nani hana huruma kwenye dunia hii hadi anaamua kuua? Nani atanipenda tena kama ulivyokuwa wewe Mashaka? Huna baya Mashaka kwenye hii dunia. Walimwengu jamani. Nirudishieni Mashaka wangu..."**

Baadhi ya abiria alidandia mabasi ili kujikoa. Wengine walitelemka kwa kudhani uwapo wao kwenye mabasi unaweza kuwa hatari kwao.

Mwili wa mtu mmoja ulilala kando ya barabara ya Kawawa. Karibu kabisa na kituo cha mabasi ya Magomeni Mikumi, upande ambao mabasi yanatoka Makumbusho, Mwenge, Kinondoni, kuelekea Mbagala, Buguruni na Gongolamboto.

Watu walipotuliza akili zao, waligundua kuwa kuna kijana mmoja alipigwa risasi moja ya kichwa iliyotosha kabisa kutoa uhai wake.

Mama mmoja masamaria mwema aliamua kutoa khanga yake moja aliyokuwa nayo na kufunika maiti.

Pamoja na kwamba kulikuwa na kinamama waliokuwa wakilia na kutokwa machozi kutokana na tukio la kikatili jinsi lilivyotokea, kuna dada mmoja alionekana kulia zaidi kuliko wengine. Alilia na kuomboleza.

"Mashaka wangu weee, Mashaka unaondoka unaniacha na nani? Mashaka amka basi kidogo nikubusu. Mashaka nani hana huruma kwenye dunia hii hadi anaamua kuua? Nani atanipenda tena kama ulivyokuwa wewe Mashaka? Huna baya Mashaka kwenye hii dunia. Walimwengu jamani. Nirudishieni Mashaka wangu..."

Ilikuwa ni sauti ambayo kila mmoja kwenye umati uliokusanyika aliposikia, alijua kuwa dada huyo ana uhusiano na kijana aliyepigwa risasi. Walichofanya wanawake waliokuwa hapo ni kumchukua, kumuweka chini na kumpa huduma zote zinazotakiwa, ikiwamo kumzuia kukurupuke na kukimbia ovyo kutokana na kuwa tayari alikuwa ameshaathirika kisaikolojia, hivyo anaweza kugongwa na gari.

Kingine ilikuwa kumbembeleza na kumliwaza ili kumweka sawa kiakili ili kuwapa nafasi wanamume waliokuwapo hapo kufanya majukumu yao sawia.

Gari la polisi lilifika hapo na baada ya kuchukua maelezo kutoka kwa watu wawili watatu, hasa wafanyabiashara waliokuwapo hapo na kuubeba mwili wa marehemu kwa ajili ya kwenda kuufanyia uchunguzi.

"Wewe unaitwa nani?" Mwanamke mmoja aliuliza. "Cecilia." Alijibu kwa sauti ndogo na kavu. Hii ni baada ya kulia hadi nguvu zikawa zimemuishia. "Basi ingia kwenye gari."

Cecy aliingizwa kwenye gari la polisi, baada ya kudokezwa kuwa mwanadada huyo ndiye alikuwa na marehemu mara ya mwisho wakiwa wamesimama kituoni kabla ya mwenzake kutandikwa shaba.

****************************

Alidhamiria kufanya chochote ili kumbakisha Cecy kwenye mikono yake. Kitendo cha kujua kuwa mpenzi wake huyo ana mwanamume ambaye kabla ya kuwa naye walikuwa wapenzi, lakini kwa sasa anaonekana kurejesha tena penzi kwa mwanaume huyo, kwake ilikuwa kama dhihaka na dharau.

Kila anapopiga simu Cecy hapokei. Na hata akimtumia ujumbe mfupi wa maandishi, uwe wa mahaba au vitisho, mwenzake hajibu. Hasira iliyochanganyikana na wivu vilimfanya Zahir kugeuka mnyama.

Alikuwa na silaha ambayo alikuwa akiimiliki kihalali. Alikuwa na uwezo mkubwa wa kulenga shabaha. Aliimiliki silaha hiyo kwa lengo la kujilinda. Siku hiyo alipata wazo la kumpigia rafiki yake Getrude. Hakutaka kujifanya kama kwa siku za karibuni wamekuwa hawana mahusiano mazuri, ila akamdanganya kuwa siku yake haipatikani.

"Kapita hapa, kasema anakwenda Magomeni Sokoni kuna kitu anakwenda kununua. Hajaniambia, kitu gani kwa hiyo mimi navyojua amekwenda huko.

Haraka."

Kabla hata hajakata simu, aliwasha gari lake kutoka nyumbani kwake Mtoni Mtongani kwenda Magomeni Sokoni. Lengo ni kubahatisha kama atamwona au la. Alipofika maeneo hayo hakufanikiwa.

Wakati akikaribia kukata tamaa kwa mbali aliona mtu kama Cecy akivuka barabara. Gari la Zahir lilikuwa kwenye foleni. Macho yake yaliona vizuri zaidi tukio hilo. Ni kwamba Cecy alikuwa akitoka kwenye mtaa uliotoka kwenye soko la Magomeni na alikuwa akivuka barabara kwenda upande wa pili. Hakuwa peke yake kwani wakati akivuka barabara alikuwa ameshikana mikono na mwanamume.

Jinsi walivyoongozana, wakiwa na tabasamu na bashasha, hata kipofu angejua kuwa ni wapenzi.

"Huyu ndiye Mashaka. Leo atanitambua. Wewe ndiye adui yangu namba moja hata duniani" Alijisemea akiwa na hasira zilizokaribia kuupasua mwili na moyo wake.

Alijipapasa mfukoni, bastola yake ilikuwapo. Akili ilikuwa imemruka. Alikuwa akitamani sehemu ambayo yule kijana yupo, awepo yeye. Alikuwa kama akiota ndoto mbaya.

"Cecy, kumbe hicho ndicho kibwana chako kinachokuzuzua, sasa ngoja nikiondoe duniani. Huyu ndiye adui yangu namba moja kwa sasa. Nikimuua tu basi. Utakwenda kwa nani. Ni lazima utarudi kwangu tu. Hutokuwa na janja tena." Alisema kwa sauti ndani ya gari, lakini alikuwa peke yake. Alijiambia mwenyewe.

Mapozi ya wapenzi hao walizidi kumtia uchizi Zahir, foleni ilinanza kutembea. Alichofanya kuliweka gari pembeni, akatelemka. Akatembea taratibu huku macho yake yakiwa mbele ili asipoteze mawindo yake.

Mashaka na Cecy, tayari alikuwa wamefika kituoni. Ilikuwa majira ya saa 12:00 jioni. Kulikuwa na umati mkubwa wa watu kituoni hapo. Kila mmoja alikuwa na mambo yake. Hakuna aliyekuwa akimfuatilia mwenzake anafanya nini.

Mashaka na Cecy tayari walikuwa wamesimama kituoni, lengo ni kupanda basi kwenda Ilala Mchikichini kufuata mahitaji ambayo waliyataka.

Walikuwa wakilishana tambi walizonunua pembeni kwa barabara. Hakuna aliyemwona Zahir ambaye aliwapita ghafla na baadaye kuvuka barabara. Akasimama katikati ya barabara mbili za Kawawa. Akatoa bastola na kumlenga Mashaka. Akaachia risasi moja tu, iliyomrusha hatua kadhaa nyuma na kuzua tafrani kituoni hapo.

Alichofanya ni kuvuka barabara ya upande wa pili. Akisaidiwa na kelele watu, kila mtu akihamanika na kukimbia ovyo. Alivuka tena barabara mbili haraka, akalifuata gari lake na kuondoka kwenda kwenye makutano ya barabara ya Kawawa na Morogoro, akakata kulia kuelekea Kariakoo. Akatokomea.

*Itaendelea Jumapili*

## HABARI BURUDANI



# KAOLEWA! ASHA BOKO APATA MUME

NANI kasema haolewi? Ndivyo wapambe walivyokuwa wakiimba wakati wa harusi ya mwigizaji mkongwe Asha Boko, ambaye ameolewa kwa mara ya pili.

Ndoa hiyo kati yake na mumewe Duwa Msafiri imefungwa kisiri Novemba 20, mwaka huu nyumbani kwao Mlanzidi mkoa wa Pwani.

Akizungumza na EATV , Asha Boko amesema hakutaka ndoa yake ijulikane kwa sababu watu wangeweza kutia vizuizi.

"Ni kweli nimeolewa leo nyumbani kwetu Mlandizi, mume wangu anaitwa Duwa Msafiri na kesho kutakuwa na sherehe ukumbini maeneo ya Bagamoyo, nilikuwa sijatangaza kwa sababu nisingeolewa watu wangenitangaza ila taarifa nimetoa kwenye familia, ndugu, jamaa na marafiki, mume wangu sio mtu maarufu hawawezi kumuiba kwa sababu anajielewa" amesema Asha Boko.

Asha Boko amefunga ndoa hiyo ikiwa ni mara yake ya pili baada ya mume wake wa kwanza kufariki dunia baada ya kushambuliwa na majambazi mwaka 2010.



# Mhh! Gigy Money sijui atakuelewa mchungaji

MWIGIZAJI wa filamu ambaye kwa sasa amemgeukia Mungu na kuwa Mtumishi, Asnath Mathias, amesema anatamani kufanya maombi kwa Gigy Money, ili kubadilisha vitendo vyake anavyovifanya katika mitandao ya kijamii.

Asnath amesema Gigy Money, ni mwanamke mzuri sana ila hapendezewi na maisha aliyokuwa nayo na amemshauri amuombee ili aanzishe maisha mapya, atulie na ajiheshimu.

"Kuokoka sio kuwa na shida na mtu bali ni kuacha mambo ya kidunia na kufanya kitu ambacho kitampendeza Mungu, Gigy Money ni mwanamke mzuri mno atambue hilo, lakini ukifungua mitandao lazima utamuona na unaona vitu vya ajabu ambavyo anavifanya na watu wanavyomzungumzia" amesema

# Stamina anapomtambua Profesa Jay



MWANAMUZIKI wa HipHop, Stamina, amesema msanii na mwanasiasa Prof Jay, anatakiwa apewe heshima ya kipekee kutokana na ushawishi wake kwa wasanii wengine.

Stamina amesema hakuna msanii wa sasa ambaye hajamsikiliza Prof Jay, wakati anakuwa au kujiandaa kuingia kwenye muziki wa BongoFleva mpaka kufikia sasa..

"Prof Jay ni kaka yangu au baba ana nafasi hiyo kwangu, kuna muda nikipiga naye stori namwambia simuoni kama mpinzani ila namuona kitaifa zaidi ila tunatakiwa kuheshimu uamuzi na maisha lazima yaendelee, nimefika hadi studio za Mwanalizombe Mikumi na nina ngoma naye"

"Hakuna rapa yeyote ambaye hajawahi kumsikiliza Prof Jay, ni mmoja kati ya inspiration kubwa kwa watu pia alibadilisha akili za wazee wetu kwamba muziki sio uhuni,kwenye maisha muogope sana mtu anayepambania watu wengine", ameongeza.

Prof Jay ni mmoja kati ya wasanii wa kwanza na wenye heshima kwa kuanza muziki hapa nchini Tanzania ambapo amefanikiwa kutengeneza ngoma kali ambazo zilifanya vizuri kwenye 'chart' na kubeba tuzo mbalimbali.




# VIRGIL

## AANZA MAZOEZI MEPESI LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Liverpool imepokea habari njema baada ya mlinzi wake, Virgil Van Dijk, kuripotiwa kuanza kufanya mazoezi mepesi yatakayomsaidia kurejea kwenye ubora wake wa zamani.

Beki huyo wa kati anasumbuliwa na majeraha ya goti ambapo kwa sasa anapambana ili arejee uwanjani baada ya kugongana na golikipa wa Everton, Jordan Pickford wakati timu hizo zilipokutana mwezi uliopita.

Baada ya kufanyiwa upasuaji Van Dijk, taarifa zinaeleza ameanza kufanya mazoezi mepesi ambayo yatamfanya aweze kurejea kwenye kikosi cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England chini ya Jurgen Klopp.

Taarifa kutoka Liverpool imeeleza kuwa beki huyo anaendelea vizuri na upasuaji wake ulikwenda vyema jambo ambalo limemfurahisha Klopp ambaye amesema wanatarajia kuwa na habari njema hivi karibuni.

Liverpool inapambana kutetea taji la ligi hiyo ikiwa inawakosa nyota wake wengi ambao ni mabeki ikiwa ni pamoja na Joe Gomez, Fabinho ambao wanasumbuliwa na majeraha.

# ZIDANE AKATAA VARANE KUUZWA



**MADRID, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesisitiza mlinzi wake, Raphael Varane hauzwi huku akihusishwa na Manchester United.

United imekuwa ikimwania kwa muda mrefu Varane na miamba hao wa Ligi Kuu England wameripotiwa wanajiandaa kutoa ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 ambaye ni raia wa Ufaransa.

Lakini Zidane ametupilia mbali uvumi huo kuhusu majaliwa ya Varane pale Santiago Bernabeu, ambako Mfaransa huyo ameshinda mataji matatu ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipotua pale mwaka 2011.

"Sio mimi tu ambaye nataka kumbakiza hapa," amesema Zidane akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana Jumamosi dhidi ya Villarreal.

"Yeye ni sehemu ya klabu hii, tulikuwa na bahati kuwa naye hapa Madrid.

"Na kiwango cha kuvutia, amepata mafanikio mengi tangu amekuja hapa. Bila shaka yoyote yeye hauzwi"

# Solskjaer: Najua Pogba hana furaha

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anatambua, Paul Pogba hana furaha lakini amesisitiza kiungo huyo ana "ubora" wote wa kurudisha kiwango chake kwa miamba hao wa Ligi Kuu England.

Majaliwa ya Pogba yamepamba vyombo vya habari baada ya Kocha Mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps, kubainisha kiungo huyo haridhishwi na hali jinsi ilivyo pale Old Trafford baada ya kuwa na wakati mgumu wa kurudisha kiwango chake.

Mfaransa huyo ambaye aling'ara kwenye mechi zote tatu za Les Bleus hao, ameanza katika mechi nne tu kati ya saba za United kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Kwenye mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya, Pogba alitajwa mara moja tu kwenye kikosi cha kwanza cha Solskjaer.


Alipoulizwa kuhusu Pogba baada ya kuhusishwa na Juventus na mabingwa wa LaLiga, Real Madrid, Solskjaer aliwaambia waandishi wa habari: "Mara zote tunapata maswali na tunajaribu kuyajibu kadiri tunavyoweza.

"Nafikiri wengi mnapenda kujua kuhusu Pogba, lakini ukweli ni kwamba najua hawezi kuwa na furaha kwa hali yake kwa sasa.

"Lakini ana ubora wote wa kumwezesha kurudisha kiwango chake. Nimezungumza na Paul kuhusu hilo na ninaamini mambo yatakwenda sawa tu."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA ATAKA MESSI KUSTAAFIA SOKA BARCA

**Kocha huyo afunguka hayo baada ya mshambuliaji huyo kuhusishwa na tetesi za kumfuata...**

**MANCHESTER, ENGLAND**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema angependelea kumwona nyota wa miamba ya soka Hispania, Barcelona na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, akimalizia soka la ushindani katika klabu hiyo.

Messi amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na City na Guardiola ambaye alimnoa wakati akiwa pale Katalunya.

Guardiola ambaye amesaini mkataba mpya wa miaka miwili ndani ya matajiri hao wa Jiji la Manchester siku ya Alhamisi, amekuwa akihusishwa kutua Barcelona na taarifa nyingine zikisema kuwa wanataka kuungana.

Mkataba wa Messi unamalizika mwishoni mwa msimu huu na inatajwa kuwa City na Paris St-Germain zitakuwa kwenye nafasi za kutuma ofa zao. Lakini Guardiola amesema: "Messi ni mchezaji wa Barcelona na ningependa amalizie soka lake pale."

"Kwa sasa sio jambo zuri kumhusisha na Manchester City, kwa sasa yeye ni mchezaji wa Barcelona," alisema Guardiola akinukuliwa na Daily Mail.

"Nimelisema hilo zaidi ya mara elfu moja sasa. Kama shabiki wa Barcelona, mshabiki wa Messi ningependa kumwona anabakia pale".

## KWA UFUPI

**SANCHEZ ANUKIA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inajiandaa kufanya usajili Januari na inaweza kumnasa mlinzi wa kimataifa wa Colombia, Davinson Sanchez mwenye umri wa miaka 24. **(Football Insider)**

**KOEMAN KUMBAKISHA MESSI**
KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman bado ana matumaini kwamba ataweza kumshawishi, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33 kubakia klabuni hapo. **(Goal)**

**KLOPP HATIHATI KUSAJILI**
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema hana uhakika kama mabingwa hao wa Ligi Kuu England watasajili beki mpya katika dirisha la Januari. **(Goal)**

**SCHUURS AWEKWA SOKONI**
LIVERPOOL imeambiwa inatakiwa kulipa pauni milioni 26.7 kama wanataka kumsajili mlinzi wa Ajax, Perr Schuurs mwenye umri wa miaka 20, huku AC Milan pia ikimwania beki huyo wa kati wa Uholanzi. **(Sempre Milan via Liverpool Echo)**

**ANCELOTTI AMKATAA ISCO**
KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, amekanusha uvumi wa kutaka kuwasajili wachezaji wawili kutoka Real Madrid, Isco mwenye umri wa miaka 28 na kiungo wa Juventus, Sami Khedira mwenye miaka 33. **(Liverpool Echo)**

**KHEDIRA ANUKIA WEST**
KLABU ya West Ham imatajwa kuwa kwenye mbio za kuwania kumsajili kiungo wa Juventus na Ujerumani, Sami Khedira mwenye umri wa miaka 33. **(Sport Mediaset, via Team Talk)**

**XHAKA HAONDOKI INTER**
KIUNGO wa kimataifa wa Uswisi, Granit Xhaka, mwenye umri wa miaka 28, hana mpango wa kuondoka Arsenal kwenda Inter Milan wakati wa dirisha dogo la usajili Januari. **(Calciomercato via Mirror)**

**RODRIGUEZ AKANUSHA KUGOMBANA**
KIUNGO wa kimataifa wa Colombia, James Rodriguez (26), amekanusha ripoti kwamba alihusika kwenye ugomvi kwenye vyumba vya kubadilishia nguo akiwa kwenye mechi za kimataifa. Nyota huyo wa Everton aliripotiwa kukwaruzana na Jefferson Lerma |(26), anayekipiga Bournemouth na nyota wa Tottenham, Davinson Sanchez ambaye ana umri wa miaka 24. **(Star)**

**RYENA AJIFUNGA DORTMUND**
KIUNGO wa kimataifa wa Marekani, Giovanni Reyna mwenye umri wa miaka 18, ambaye amekuwa akihusishwa na Liverpool amesaini mkataba wa muda mrefu na Borussia Dortmund. **(Team Talk)**

**EPL YAMVUTIA HAALAND**
BABA mzazi wa Erling Haaland, Alf-Inge ambaye ni mchezaji wa zamani wa Nottingham Forest, Leeds na Manchester City, amekubali nyota huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 20, anavutiwa na Ligi Kuu England. **(Sport 1, via Mirror)**

**MESSI ATABIRIWA CITY**
KIUNGO wa zamani wa Manchester City, Trevor Sinclair, anaamini ujio wa nyota wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33 pale Etihad unawezekana baada ya Pep Guardiola kusaini mkataba mpya. **(Talksport)**

**KENT AKARIBIA LEEDS**
LEEDS United inatarajia kuwasilisha ofa ya pauni milioni 20 kwa ajili ya kumnasa winga wa Rangers, Ryan Kent (24), kama nyota huyo atashindwa kufikia muafaka na klabu yake hiyo maarufu kwa jina ya Ibrox. **(Football Insider)**



HABARI MICHEZO

# MKWASA AUPOTEZEA UBINGWA WA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kuendelea kuwa na matokeo mazuri dhidi ya wapinzani wao, Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, amesema hafikirii kukipa nafasi kikosi chake ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo wa zamani wa Yanga amesema malengo yao ni kuona wanamaliza msimu huu kwenye nafasi tano za juu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkwasa alisema wamefanya maandalizi ya kupambana na ushindani na vile vile kutafuta matokeo mazuri katika kila mechi ili kumaliza kwenye nafasi nzuri.

Alisema mikakati yao ni kuhakikisha timu hiyo inapata matokeo mazuri katika mechi hizo na ikatokea akapoteza ana imani ni suala la mpira ambalo lipo.

"Kwa sasa tunafikiria kutafuta matokeo katika mechi ili kumaliza ligi bila ya presha, kwa msimu huu hatuna wazo la ubingwa sababu ya maandalizi tuliyoyafanya mwanzoni mwa msimu huu, kwa ajili ya kutafuta matokeo ambayo tutaendelea kubaki katika ligi pamoja na kuandaa vijana," alisema Mkwasa.

Aliongeza uamuzi wa kuwaamini wachezaji vijana umeisaidia kufanya vyema na ataendelea kuwapa nafasi kwa sababu timu hiyo inasimamiwa na taasisi ambayo haina uwezo wa kusajili nyota wa kulipwa ambao wanahitaji kulipwa gharama kubwa.

"Kuwaamini vijana katika timu yangu na kunipa matokeo mazuri ni jambo la kujivunia, hii sio kwa ajili ya Ruvu pekee pia watakuja kutusaidia hapo baadaye katika timu zetu za Taifa watakapoonekana na kuaminika," alisema Mkwasa.

Aliongeza kikosi chake kinaendelea kuimarika na vijana hao kumpa matokeo mazuri ikiwamo ushindi wa juzi dhidi ya Mbeya City, nyota wake wanazidi kuimarika na wanajiamini kwa ajili ya kupata ushindi kwenye mechi zinazofuata.

Ruvu Shooting juzi ilipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mbeya City na kupaa hadi kwenye nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufikisha pointi 19.



Wasanii wa Kikundi cha Ngoma za Asili cha Simba Theatre Art International, wakitoa burudani katika uzinduzi wa bodi mpya ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), na kuiaga bodi iliyomaliza muda wake jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kagere, Miquissone warejea nchini

**Na Saada Akida**

NYOTA wawili wa kimataifa wa Simba mshambuliaji, Meddie Kagere na winga, Luis Miquissone, wamerejea nchini wakitokea kuzitumikia timu zao za Taifa za Rwanda na Msumbiji, tayari kuanza maandalizi ya kuwavaa Plateau United ya Nigeria katika mechi ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kagere na Miquissone walikosa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi Coastal Union uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha baada ya kuchelewa kurejea nchini.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck alisema anatarajia wachezaji hao watakuwapo katika msafara wa kuelekea Nigeria na tayari kwa mchezo wao huo wa kwanza wa kimataifa.

"Walichelewa kujiunga na timu kwa kuwa walikuwa na majukumu kwenye timu zao za Taifa, wataungana na kikosi mapema na watakuwa miongoni mwa wachezaji watakaokuwa katika majukumu ya klabu kwenye michuano ya kimataifa," alisema Sven.

Kagere ambaye alikuwa majeruhi ameliambia gazeti hili sasa yupo fiti kwa ajili ya kurejea uwanjani na katika kuhakikisha timu yake inafanya vizuri katika mechi zote zinazowakabili.

"Baada ya kukaa nje muda mrefu na kupata matibabu, sasa niko fiti na nipo tayari kurudi uwanjani kusaidia timu yangu kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Kagere.

Kagere ametua nchini juzi akitokea Rwanda, wakati Miquissone ameungana na kikosi hicho jana.

Simba itavaana na Plateau United katika mchezo wa kwanza utakaochezwa kati ya Novemba 27 na 29, mwaka huu huku ikiwakaribisha wageni hao Desemba 6 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini.

## Ngorongoro kamili kuwavaa Djibouti

**Na Anthony Benedictor**

WENYEJI Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), inatarajia kuwavaa yosso wenzao wa Djibouti katika mechi ya ufunguzi ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20), itakayofanyika leo kwenye Uwanja wa Black Rhino ulioko Karatu jijini, Arusha.

Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Jamhuri Kihwelo 'Julio' alisema kikosi chake kiko tayari kwa mashindano hayo na wamejipanga kutetea ubingwa wanaoushikilia baada ya kupangwa Kundi A pamoja na Somalia.

Julio alisema wanatarajia kukutana na ushindani kwa sababu timu zote zimefanya maandalizi imara.

Julio alisema amejiandaa kukutana na ushindani na kundi lake lina timu zenye upinzani kutokana na kuziona kwenye mechi za kirafiki.

"Tumeona makundi na kuwaona wapinzani wetu, kama ilivyo awali tunahitaji kutetea ubingwa wetu na kuwa miongoni mwa timu ambazo zitasonga mbele kuwania tiketi ya kufuzu moja kwa moja michuano ya Afrika (Afcon U-20," alisema Julio.

Aliongeza kwa kuwaomba mashabiki wa soka wa Arusha kujitokeza kuwashangilia wawakilishi wao ili kuwaongezea hamasa ya kufanya vyema.

Ngorongoro Heroes itashuka tena dimbani Alhamisi Novemba 26, mwaka huu kuwakabili Somalia na timu itakayoongoza kwenye kundi hilo itatinga hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo.

## JKU FC, Kipanga hakuna mbabe

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU imeshinda kutamba baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Kipanga katika mechi ya ufunguzi ya msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan juzi.

Katika mchezo huo, timu zote zilionekana imara kwenye safu za ulinzi, jambo ambalo lilipelekea dakika 90 kumalizika huku kila upande ukishindwa kuliona goli la mwenzake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa JKU, Omar Khamis "Kocha Matu" alisema matokeo ya sare katika mchezo huo yamesababishwa na makosa yaliofanywa na washambuliaji ambao walipoteza nafasi walizozitengeneza.

Alisema washambuliaji wake walikosa umakini katika kufunga magoli lakini aliwasifu wapinzani wao walijipanga vyema kuhakikisha wanaimarisha safu yao ya ulinzi katika dakika zote za mchezo huo.

"Tuilijitahidi kucheza vizuri lakini tulikosa umakini pale nafasi ilipopatikana, wachezaji walijituma walijaribu kupeleka mashambulizi kila wanapopata mpira, lakini walishindwa kutikisa nyavu za wapinzani wetu, tutajipanga katika mchezo wetu ujao ambao tunakutana na KMKM," alisema kocha huyo.


Katika mechi nyingine iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau A, Black Sailor ilianza vyema ligi hiyo kwa kupata alama tatu baada ya kuifunga KVZ mabao 2-1.

Ligi Kuu Zanzibar itaendelea tena leo kwa Mlandege kuwakaribisha Hard Rock kutoka Pemba kwenye Uwanja wa Mau A wakati Zimamoto itavaana na KMKM Uwanja wa Amaan.

# Michezo

Jumapili Novemba 22, 2020

Nipashe



## Guardiola ataka Messi kustaafia soka Barca

HABARI UK 22

# Yanga, Namungo mechi ya hesabu

**Na Saada Akida**

USHINDI ndio neno kubwa la Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi saba, sare tatu na ndio timu pekee haijapoteza mchezo wakati Namungo imeshinda michezo minne, sare mara mbili na kufungwa mara nne.

Kaze aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanaendelea na kasi waliyokuwa nayo kabla ligi hiyo haijasimama.

Kocha huyo alisema amefurahi nyota wake waliokuwa majeruhi akiwamo beki tegemeo, Lamine Moro wamepona na hivyo ana nafasi nzuri ya kupanga kikosi anachotaka.

"Kila mechi ina mpango wake, tulivyocheza dhidi ya Biashara, si tutakavyocheza kesho (leo), dhidi ya Namungo, ila najua mechi itakuwa ngumu, Ligi ya Tanzania ina ushindani mechi zote, tofauti ni majina tu ya klabu," Kaze alisema.

Aliongeza kwa kuwataka viungo wake kubadilisha mbinu ili iwe rahisi kwao kupata ushindi katika mchezo huo na katika idara hiyo anawategemea zaidi Farid Mussa na Carlos Carlinhos.

Mzanzibari Hemed Morocco ataiongoza Namungo kwa mara ya kwanza baada ya kurithi mikoba ya Hitimana Thiery ambaye ametimuliwa kwenye klabu hiyo.

"Ninaifahamu Ligi Kuu, sio mgeni, ninaamini nitaibadilisha timu na kufikia malengo yaliyokusudiwa, tutakuwa na kipindi cha mpito lakini hili ni jambo la kawaida katika klabu za mpira," alisema Morocco.

Mechi nyingine ya ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Kagera Sugar dhidi ya Mwadui FC kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (katikati), akijiandaa kuwatoka wachezaji wa Coastal Union katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha jana. Simba ilishinda mabao 7-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YATUMA SALAMU NIGERIA

## Bocco apiga 'hat-trick' wakati Mnyama akiisulubu Coastal Union mabao 7-0, Azam hoi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

NAHODHA wa Simba, John Bocco, amefunga 'hat-trick' yake ya kwanza msimu huu huku mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakitoa kipigo kizito cha mabao 7-0 kwa Coastal Union katika mchezo uliofanyika kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha jana.

Baada ya mechi ya jana, Simba itaendelea na maandalizi ya kuwafuata Plateau FC ya Nigeria kwa ajili ya mechi ya kwanza ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa mwishoni mwa wiki.

Kwa mabao hayo, Bocco anakwea hadi kileleni katika orodha ya wafungaji msimu huu baada ya kufikisha mabao saba, akiwaacha, Prince Dube wa Azam FC na Adam Adam wa JKT Tanzania ambao wana magoli sita kila mmoja.

Kwenye mechi hiyo, winga wa Simba, Bernard Morrison, alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu Bara msimu huu, lakini pia ni bao lake la pili kwa timu hiyo, akifanya hivyo kwenye uwanja huo huo, alifunga bao la pili kwenye mechi ya Ngao ya Jamii iliyochezwa Agosti 30, mwaka huu, Simba ikiichapa Namungo mabao 2-0.

Hii si mara ya kwanza, kwani misimu miwili iliyopita, 2018/19, Coastal ilipata kichapo cha mabao 8-0 kutoka kwa Simba kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, mechi iliyochezwa Machi 8, mwaka 2019. Dalili za Simba kupata mabao mengi, zilianza kuonekana mapema tu kwenye dakika ya nne, wakati mabeki wa Coastal Union walipomsahau kiungo, Hassan Dilunga wakidhani ameotea, lakini alikokota sana na kuchelewa kupiga, akakutwa na mabeki wa timu hiyo wakaokoa kabla hajafanya kitu chochote.

Dilunga alirekebisha makosa yake dakika mbili baadaye alipopachika bao la kwanza, kufuatia 'kumlamba' chenga kipa wa Coastal Union, Aboubakar Abbas na kuujaza wavuni, baada ya kupata pasi kutoka kwa nahodha wake, Bocco. Faulo la dakika ya 14 iliyopigwa na Claotus Chama, nusura ilipatie Simba bao ilipogonga nguzo na kurejea uwanjani, huku kipa Abbas akiwa ameshakubali matokeo.

Kuanzia dakika ya 24, Bocco alianza kufanya shughuli yake, kwa kupachika bao la pili kwa Simba, akimalizia pasi safi kutoka kwa Diunga na wakati wachezaji wa Coastal wakishangaa, wasijue nini kimetokea, dakika mbili baadaye Bocco tena alifunga bao la tatu ambalo lilitokana na kupokea pasi kutoka kwa Morrison.

Nahodha huyo aliingia kwenye orodha ya kuwa mfungaji wa pili wa 'hat-trick' msimu huu baada ya Adam Adam wa JKT Tanzania, kwenye dakika ya 39, alipoupata mpira akiwa katikati ya mabeki wawili wa Coastal Union, akageuka na waacha huku wakimsukuma, lakini alipepesuka na alipokaa sawa, alitisha mara mbili kama anapiga, ya tatu akaachia shuti la juu lililokwenda moja kwa moja hadi wavuni.

Adam alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga 'hat-trick', Oktoba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mwadui Complex, alipofunga mabao matatu katika mchezo uliomalizika kwa JKT Tanzania kushinda mabao 6-1 dhidi ya wenyeji, Mwadui FC.

Inaonekana kama Uwanja wa Sheikh Amri Abeid unampenda Morrison, kwani alirejea tena hapo na kufunga tena bao dakika ya 45 likiwa ni bao la tano, alipoupata mpira pembeni, kauweka kifuani kabla ya kuvuta hatua kadhaa na kuachia shuti la 'mwandamo wa mwezi' lililojaa pembeni mwa goli, ukimshinda kipa Abbas. Kipindi cha pili kilipoanza, Kocha Sven Vandernbroeck, alimpumzisha Bocco na nafasi yake kuchukuliwa na Ibrajim Ajibu ambaye alitoa pasi ya kisigino dakika ya 59 kuelekea kwa Chama, akiwa ndani ya eneo la hatari alipiga shuti hafifu kwa mguu wa kushoto na kuandika bao la sita.

Ni chama tena aliyepigilia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Coastal Union, alipofunga bao la saba dakika tano kabla mechi kumalizika kwa mkwaju wa faulo, iliyotokana na Morrison kuangushwa nje kidogo ya eneo la hatari.

Kwa matokeo hayo, Simba inafikisha pointi 23, magoli 29 ya kufunga, ikifungwa matano, lakini ikiendelea kuwa kwenye nafasi ya tatu nyuma ya Azam na Yanga, huku Coastal Union ikiwa kwenye nafasi ya 13 kwa pointi 12, timu zote zikiwa zimecheza mechi 11.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, KMC imeibuka na ushindi wa bao 1-0, dhidi ya Azam FC na goli hilo pekee likifungwa dakika ya 59 na Reliant Lusajo aliyeunganisha pasi ya Kelvin Kijiri. Timu zote zilifanya mashambulizi mbalimbali lakini Azam wataendelea kukumbuka shuti la dakika ya 25 la Prince Dube ambalo liligonga mwamba wa juu na dakika moja baadaye alikosa nafasi nyingine kwa mpira wa kichwa aliopiga kugonga mwamba wa chini.

Polisi Tanzania yenyewe ililazimishwa sare ya bila kufungana na Ihefu katika mechi iliyochezwa mapema jana mchana kwenye Uwanja wa Azam Complex.

9 770856 541002 >